Haliuzwi
FEBRUARI 17, 2026
/islamicftz
Ramadhan 1 1447
IMAAN
ISSN 5618 - NO. 571
Huwatoa watu gizani kwa idhini ya Allah

Israel kudhibiti Waislamu kuingia Masjid Aqsa Ramadhan hii

Ramadhan Mubaarak

- **WAISLAMU NCHINI TANZANIA** wanaungana wenzao duniani kote kuanza mfungo wa mwezi mtukufu wa Ramadhan, leo Jumatano, Februari 18, 2026 sawa na tarehe Mosi Ramadhan mwaka 1447H
- Kuonekana kwa mwezi kumethibitishwa kupitia taarifa rasmi iliyotolewa na Kamati ya Mwandamo ya Baraza la Sunna Tanzania (BASUTA) na kusainiwa na Mwenyekiti wake, Sheikh Salim Barahiyan.

SHEIKH IBRAHIM TWAHA:

Ramadhan sio kushinda na njaa, ni uchamungu

Tamasha la Makka Halal Forum 2026 lanoga

Bajeti mpya Zanzibar kufikia Sh8.217 trilioni

Mwinyi: Taasisi za kidini nguzo ya amani na maadili ya jamii

UN: Tanzania ina mifumo imara ya maridhiano

Ramadhan ya tatu mfululizo Wapalestina wangali katika mateso

رمضان مبارك
RAMADHAN MUBARAK
Mwenyekiti wa The Islamic Foundation, AREF NAHDI;
Mkurugenzi Mtendaji, SHEIKH IBRAHIM TWAHA;
Mkurugenzi wa Imaan Media , MUHAMMAD MATANO;
na watendaji wake wote wa taasisi, wanawatakia
watazamaji wa TV Imaan, wasikilizajii wa Redio Imaan,
wasomaji wa Gazeti Imaan na Waislamu wote duniani
mfungo mwema wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhan 1447.
The Islamic Foundation

UKHTI FATIMA SS

RAMADHAN MUBAARAK

Waislamu waanza kufunga

WAISLAMU NCHINI TANZANIA wanaungana wenzao duniani kote kuanza mfungo wa mwezi mtukufu wa Ramadhan, leo Jumatano, Februari 18, 2026 sawa na tarehe Mosi Ramadhan mwaka 1447H.

Kwa siku 29 au 30, Waislamu zaidi ya bilioni 1.8 duniani watajizuia kula na kunywa kuanzia alfajiri hadi machweo ya jua, kufuatia kuthibitishwa kuonekana kwa mwezi mwandamo Jumanne jioni katika Ufalme wa Saudi Arabia, Yemen, Umoja wa Falme za Kiarabu na nchi nyingine kadhaa za Kiislamu.

Kuonekana kwa mwezi huo ndiko kunakoashiria rasmi kuanza kwa mwezi wa Ramadhan katika kalenda ya Kiislamu ya mwandamo.

Kwa Tanzania, taarifa za kuonekana kwa mwezi zimethibitishwa kupitia taarifa rasmi iliyotolewa na Kamati ya Mwandamo ya Baraza la Sunna Tanzania (BASUTA) na kusainiwa na Mwenyekiti wake, Sheikh Salim Barahiyan.

Ramadhan ni mwezi wa tisa katika kalenda ya Kiislamu, ambayo huwa na miezi 12 na siku 354 au 355 kwa mwaka. Kufunga katika mwezi huu ni nguzo ya nne ya Uislamu na ni faradhi kwa Waislamu wote waliobaleghe na wenye afya njema.

Watoto wadogo, wagonjwa, wasafiri na wanawake wajawazito au wanaonyonyesha hupewa ruhusa maalum ya kutofunga kwa mujibu wa mafundisho ya dini.

Katika mwezi huu, Waislamu hujizuia kula, kunywa na mambo mengine kuanzia alfajiri hadi machweo ya jua, na hufuturu baada ya kuzama kwa jua. Mwezi wa Ramadhan ni kipindi cha kuongeza ibada, kusoma Qur'ani, kutoa sadaka, kusaidia wahitaji na kuimarisha mshikamano wa kifamilia na kijamii.

Mwisho wa mwezi huu huadhimishwa kwa sikukuu ya Eid al-Fitr, inayofuatia baada ya kuthibitishwa kuonekana kwa mwezi mpya wa Shawwal.

Katika nchi nyingi zenye Waislamu wengi, ratiba za kazi na masomo hupunguzwa ili kutoa nafasi kwa ibada na mapumziko. Hata hivyo, baadhi ya nchi hutofautiana tarehe ya kuanza Ramadhan kulingana na uthibitisho wa kuonekana kwa mwezi katika maeneo yao.

Waislamu nchini Tanzania wameupokea mwezi huu kwa furaha na maandalizi ya ibada, wakitarajia kuutumia kama fursa ya kujitakasa kiroho, kuimarisha maadili na kukuza mshikamano wa kijamii.



QARAAR (TAARIFA) Na.1/26 **29 SHAABAN,1447 HIJRI / 17 FEBRUARI, 2026**

YAH: TAARIFA YA KUANDAMA MWEZI WA RAMADHAN MWAKA 1447 HIJRIYA SAWA NA MWAKA 2026 MILADIYA

Baraza Kuu la Jumuia za Ansaar Sunnah Tanzania (BASUTA) linawatangazia Waislamu wote wanaofunga na kufungua kwa muandamo usiozingatia masafa maalum au mipaka ya kijiografia kwamba tumepokea taarifa ya kuthibitishwa kwa muandamo wa mwezi wa Ramadhan 1447 Hijriya kutoka Yemen, Saudi Arabia, Qatar, Bahrain, United Arab Emirates na Kuwait.

Kwa mujibu wa taarifa hizo, leo Jumanne tarehe 17 Februari 2026, mwezi umeonekana, hivyo kesho Jumatano tarehe 18 Februari 2026 ni siku ya Mosi ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhan, inshaAllah.

Mtume wa Allah (rehma na amani ziwe juu yake) anasema: "Fungeni kwa kuonekana mwezi na fungeni kwa kuonekana mwezi, na iwapo mtagubikwa na wingu (msiwee kuona mwezi), basi kamilisheni hesabu (ya mwezi) siku thelathini." (Bukhari)

Sambamba na hayo, tunawakumbusha Waislamu kujiandaa ipasavyo kwa mwezi huu Mtukufu wa Ramadhan kwa kutekeleza ibada ya Swawmu, Sala za Tarawehe, kusoma Qur-ani Tukufu, kutoa Sadaqa, na kutenda mema kwa ujumla. Mwezi wa Ramadhan ni fursa kubwa ya kujikurubisha kwa Allah Subhaanahu wa Taala.

Pia tunawakumbusha Waislamu wote kwamba mwezi wa Ramadhan ni mwezi ambao Allah Mtukufu ameuafanya kuwa bora, na ndani yake kuna Laylatul Qadr ambayo ni bora kuliko miezi elfu.

SHEIKH SALIM ABDULRAHIM BARAHIYAN
MWENYEKITI KAMATI YA MWANDAMO
BASUTA

UKHTI FATIMA SS

SHEIKH IBRAHIM TWAHA:

Ramadhan sio kushinda na njaa, ni uchamungu

Mhadhiri mbobevu, Sheikh Ibrahim Twaha Ibrahim ameuelezea mwezi mtukufu wa Ramadhan kama kituo chenye maslahi ambacho mwanadamu anatakiwa akitumie vema ili atengenekewe mambo yake ya dunia na akhera.

Sheikh Twaha, ambaye pia ni Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi ya The Islamic Foundation, aliyasema hayo katika mhadhara alioutoa katika msikiti wa Chuo Kikuu cha Waislamu cha Morogoro (MUM) wakati akiongea na jamii ya chuo hicho.

Sheikh Twaha alikosoa watu wanaoungalia mwezi huo kama mwezi tu unaopita katika kalenda, kama miezi mingine na hivyo kukosa kufaidika nao.

"Watu wengine wanaweza kuona Ramadhan sawa na kalenda tu. Imekuja Ramadhan mwaka huu, itaondoka, itakuja Ramadhan nyingine. Hapana! Ramadhan ni kituo chenye maslahi," alisema Sheikh Ibrahim.

Alisema Waislamu wakiufahamu mwezi wa Ramadhan kama kituo cha kuwarekebisha na kuwatengenezea maisha mapya (na sio mwezi katika kalenda unaokuja na kutoka), hapo ndio watakuwa wamelifahamu lengo la Ramadhan.

Akinukuu kauli ya Allah 'Azza Wajallah' aliposema: "Enyi mliyoamini! Mmeandikiwa swaumu, kama walivyoandikiwa waliokuwa kabla yenu ili mpate kumcha Mungu." [Qur'an, 2:183], Sheikh Ibrahim alisema maisha mapya ambayo Ramadhan inayotutengenezea na ambayo tunayahitaji, ni maisha ya uchamungu.

Sheikh Ibrahim alisema mchamungu hana hasara katika dunia wala Akhera kwa sababu atakuwa na wepesi katika kujibu maswali ndani ya kaburi, atafufuliwa katika hali nzuri na atapita kwa haraka katika Sirat (njia) ambayo chini yake kuna Janannam.

Ramadhan ni yetu Umma wa Muhammad

Sheikh Ibrahim aliikumbusha jamii hiyo ya MUM kuwa, licha ya kuwa umati zilizopita pia walifaradhishiwa funga; mwezi wa Ramadhan ni maalum kwa ajili ya umati wa Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani), jambo ambalo tunatakiwa tusikie fahari kuwa nalo.

Akitilia nguvu kauli hiyo, alirejea aya inayosema mwezi wa Ramadhan ndio imeshushwa Qur'an, jambo linaloonesha umaalum wa mwezi huu kwa umati wa Muhammad (Allah amshushie rehema na amani).

"Mwezi wa Ramadhan ni wetu Umma wa Muhammad (Allah amshushie rehema na amani), ila funga ni ya wote, umma zilizopita na umma wa Muhammad," alisisitiza Sheikh Twaha.

Lengo ni uchamungu

Sheikh Ibrahim alitumia mhadhara huo pia kufafanua lengo la funga ambalo ni uchamungu. Alisema mfasiri wa Quran, Imam Ibn Kathir, amefafanua neno "ili muwe wachamungu" katika aya inayotaja lengo la funga kuwa ni kuogopa maasi, na katika kubainisha ushahidi zaidi wa nguvu ya funga katika kuweka watu mbali na maasi, alimnukuu Mtume aliyewausia vijana ambao hawajapata uwezo wa kuoa kufunga.

Katika kushajiisha Waislamu kuutumia vema mwezi wa Ramadhan, Sheikh Ibrahim alinukuu hadith mbili zinazoelezea hasara ya kutoutumia mwezi huo vema.

Katika hadith ya kwanza Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema kuwa yoyote yule ambaye umeingia mwezi wa Ramadhan halafu akaharamishiwa kupata mazuri yake, basi amepata hasara. Katika hadith nyingine Mtume amesema ameangamia sana, kisha ameangamia sana kisha ameangamia sana yule ambaye ukamkuta mwezi wa Ramadhan mpaka ukaondoka na asisamehewe.

Tuupokeeje mwezi mtukufu?

Sheikh Ibrahim ametaja njia tatu ambazo watu wa hupokea mwezi wa Ramadhan, ikiwemo mbaya na isiyofaa ya kufanya maasi, maarufu kama vunja jungu (kufanya maasi ya haraka, mara ya mwisho kabla ya kutubu).

Sheikh Ibrahim wanaojihusisha na vunja jungu kuwa mwanadamu hana ahadi na Mwenyezi Mungu kuwa ataishi hadi muda huo aliopanga kutubu lakini pia huko ni kuichezea dini ya Mwenyezi Mungu.

"Katika nchi yetu Tanzania ilikuwa zamani watu wa miziki, wanaandaa shoo mbalimbali kwa ajili ya vunja jungu, lakini Waislamu wamezungumza, wamekemea, wakapaza sauti masala kama haya sasa hamna," alisema Sheikh Ibrahim.

Njia ya pili ambayo watu hupokea mwezi wa Ramadhan, kwa mujibu wa Sheikh Ibrahim, ni kwa mambo ya halali lakini yasiyo na ulazima.

رمضان

MATUKIO KATIKA PICHA

Na abdulrahman Omar

0655 763 580

Mhadhara Chuo Kikuu cha Waislamu cha Morogoro

Na Said Rajab
0783 650 803

Tutumie mwezi wa Mtukufu wa Ramadhan kwa ukamilifu!

Mwezi wa Ramadhan, ambao ni mgeni mtukufu tuliyekuwa tukimsubiri kwa hamu kubwa umeshaingia. Hiki ni kipindi cha biashara. Ndiyo, ni kipindi cha kufanya biashara na Allah 'Azza Wajallah'. Allah anasema: "Mwezi wa Ramadhan ambao imeteremshwa humo Qur'an kuwa ni muongozo kwa watu, na hoja zilizo wazi za muongozo na upambanuzi." [Qur'an, 2:185].

Tutumie mwezi wa Ramadhan kwa ukamilifu!

Mwezi wa Ramadhan, ambao ni mgeni mtukufu tuliyekuwa tukimsubiri kwa hamu kubwa umeshaingia. Hiki ni kipindi cha biashara. Ndiyo, ni kipindi cha kufanya biashara na Allah 'Azza Wajallah'. Allah anasema: "Mwezi wa Ramadhan ambao imeteremshwa humo Qur'an kuwa ni muongozo kwa watu, na hoja zilizo wazi za muongozo na upambanuzi." [Qur'an, 2:185].

Ndani ya Ramadhan malipo huzidishwa, daraja za watu hunyanyuliwa, makosa husamehewa, madhambi na matendo maovu hufutwa, na watu huachwa huru kutokana na Moto. Kuufikia mwezi huu ni baraka kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

Kuna wale ambao wameshaondoka katika ulimwengu wa matendo, na wameelekea kwenye ulimwengu wa malipo. Wangapi tunaowafahamu ambao tulifunga pamoja Ramadhan iliyopita lakini hawakufika Ramadhan hii? Hivi sasa wapo kwenye makaburi yao na matendo yao waliyoyafanya.

Wote wanatamani lau wangerudishwa kwenye maisha ya duniani, siyo kuja kulimbikiza mali au kufurahia raha zake, bali kuongeza matendo mema kwenye mizani zao. Inaonekana kama jana tu tuliiaga Ramadhan iliyopita, lakini sasa tayari tumeshaipokea Ramadhan ya mwaka huu. Subhanallah! Ni haraka kiasi gani usiku na mchana unapita, na hiyo ndiyo kasi ambayo maisha yetu yanaondoka!

Wote tumeona kwamba kile kilichopita katika maisha yetu imekuwa kama ndoto tu. Sasa fahamu kwamba kile kilichobaki katika maisha yako, nacho kitapita kwa kasi ile ile ya kile kilichopita, na kifo kitakushangaza kwa ghafla!

Utatamani kurejea tena kwenye maisha ya duniani ili utende mema. Lakini maisha ni fursa moja tu ambayo haiwezi kurudiwa. Yeyote anayefanikiwa katika mtihani huu, hakika amepata furaha kubwa na ya kweli; ya yeyote anayeshindwa mtihani huu na kupoteza maisha yake katika upotofu na uasi, basi atakuwa na majuto makubwa na masikitiko.

Allah 'Azza Wajallah' anasema: "Mpaka yanapomfikia mmoja wao mauti, husema: 'Mola wangu! Nirudishe. Ili nitende mema sasa badala ya yale niliyoyaacha. Wapi! Hii ni kauli aisemayo yeye tu. Na nyuma yao kipo kizuizi mpaka siku watakapofufuliwa." [Qur'an, 23:99–100].

Kwa hakika, mwezi wa Ramadhan ni fursa kubwa ya kuzidisha uchamungu, kumrejea Allah 'Azza Wajallah' na kumgeukia kwa ibada na toba. Ni fursa ya uwajibikaji na kujazia pale palipobaki katika maisha.

Kwa hiyo, Muislamu lazima awe makini kupanga vyema muda wake ndani ya mwezi wa Ramadhan na kuweka azimio la kutoacha siku hata moja ya Ramadhan ipite bila yeye kutenda jema, ambalo atalifurahia siku atakapokutana na Mola wake.

Muislamu azingatie kwamba Ramadhan hii inaweza kuwa ya mwisho kwake hapa duniani, hivyo awe makini kupunguza mzigo wake wa kushikamana na mambo ya dunia wakati wa Ramadhan ili atumie muda mrefu zaidi kwenye ibada.

Kwa hakika, kushikamana na mambo ya hii dunia huwa hakuishi. Kila ilipoingia Ramadhan, Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) alikuwa na bidii kubwa katika Ibada, na alikuwa rahimu zaidi kwa watu. Na zinapoingia siku 10 za mwisho alikuwa akifanya Itikaf na kujitenga kabisa na maisha ya ulimwengu ili kujielekeza kikamilifu katika kumuabudu Mola wake.

Hakika miongoni mwa hekima za kufurahia swaumu ni kuifikia 'Taqwa' (uchamungu). Allah 'Azza Wajallah' anasema: "Enyi mliyoamini! Mmeandikiwa swaumu, kama walivyoandikiwa waliokuwa kabla yenu ili mpate kumcha Mungu." [Qur'an, 2:183]. Kwa hiyo, matunda muhimu ya kufunga ni kuifikia 'taqwa'.

Mtu ambaye funga yake haimfikishi kwenye matunda hayo anapaswa kujiangalia zaidi yeye mwenyewe, kama anafunga kweli au anafanya mchezo! 'Taqwa' hujumuisha kufanya vitendo vya utii kwa Allah 'Azza wa Jallah' na kuepuka makatazo yake.

Kwa hiyo, hali ya Muislamu ndani ya Ramadhan inapaswa kuwa bora zaidi kuliko hali yake kabla ya Ramadhan. Pia, mwezi huu unapoanza, Waislamu wanapaswa kuwa makini zaidi katika ibada. Muislamu lazima azingatie kwanza yale majukumu ya faradhi, kisha baadaye aongeze vitendo vya kujitolea vya ibada. Na maeneo ya utii kwa Mwenyezi Mungu na kutenda mema yapo mengi na pia tofauti.

Hakika mwezi wa Ramadhan ni chuo cha mafunzo kwa Waislamu, ambapo wanafinyangwa kuwa na tabia njema, ikiwa ni pamoja na kujiweka mbali na madhambi na vitendo viovu. Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) amesema: "Yeyote asiyeacha maneno mabaya na kuyafanyia kazi, basi Mwenyezi Mungu hahitaji (mtu huyo) kuacha chakula chake na kinywaji chake." [Bukhari].

Maana yake, yule asiyefuata adabu za kufunga na anayetenda madhambi mengi, ambayo Mtume ameyaeleza kama 'maneno mabaya na kuyafanyia kazi', Allah hakubali swaumu yake. 'Maneno mabaya' maana yake ni madhambi ya ulimi, na 'kuyafanyia kazi' maana yake ni madhambi ya viungo.

Hivyo yeyote anayetenda madhambi hayo, ambaye hana heshima na kufunga, basi Allah 'Azza Wajallah' hana haja na kuacha kwake kula wala kunywa. Hii ina maana, licha ya mtu huyu kutekeleza wajibu wa kufunga atakosa malipo kwa sababu ya ukosefu wake wa adabu za kufunga na ujasiri wake wa kutenda madhambi.

Mtu anayefunga, anafanya mafunzo ya kuacha madhambi na kufanya matendo ya kumtii Mwenyezi Mungu kupitia shule ya kufunga, ambayo inakamilika kwa siku 30. Siku 30 zinatosha sana kwa mtu kushika tabia mpya njema na kuacha tabia mbaya. Kwa hiyo, Waislamu wanapaswa kuwa makini katika kuutumia vyema mwezi Mtukufu wa Ramadhan ili kupata tabia njema na kuachana na tabia mbaya.

Ndugu zangu katika imani, mkulima anajitahidi sana kulima, kupanda na kupalilia shamba lake, akitarajia kupata matunda ya jasho lake siku ya kuvuna. Halikadhalika, maisha haya ya duniani ni kama shamba kwa ajili ya Akhera. Kwa hiyo, panda mbegu bora ili uweze kuvuna matunda bora Siku ya Kiama: "Enyi mliyoamini! Mcheni Mwenyezi Mungu, na kila nafsi iangalie inayoyatanguliza kwa ajili ya Kesho." [Qur'an, 18:59].



NA MWANDISHI WETU

Mwinyi: Taasisi za kidini nguzo ya amani na maadili ya jamii

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Alhaj Dkt. Hussein Ali Mwinyi, amesema Serikali inatambua na kuthamini mchango mkubwa unaotolewa na taasisi za kidini katika kudumisha amani nchini.

Alhaj Dkt. Mwinyi ameyasema hayo alipoizindua Ijitimai ya Kimataifa ya kila mwaka inayoandaliwa na Jumuiya ya Fissabilillah Tabligh Markaz, inayofanyika Fuoni Migombani, Mkoa wa Mjini Magharibi.

Amefahamisha kuwa Serikali itaendelea kushirikiana na viongozi pamoja na taasisi za kidini ili kuhakikisha nchi inaendelea kubaki katika hali ya amani na utulivu, huku akiwahimiza waumini wa dini ya Kiislamu kufahamu kuwa Uislamu unasisitiza elimu, mawaidha na hekima katika maisha ya kila siku.

Aidha, Alhaj Dkt. Mwinyi ameeleza kuwa jukumu la kuamrisha mema si suala la kuwaachia viongozi wa dini pekee, bali ni jukumu la kila mmoja, na kwamba waumini wana wajibu wa kuhamasishana kutenda mema na kusaidiana.

Amewahimiza waumini wa dini ya Kiislamu kuupokea Mwezi Mtukufu wa Ramadhan kwa kuzidisha ibada na kumcha Mwenyezi Mungu, sambamba na kuwataka wafanyabiashara kuacha kupandisha bei za bidhaa za chakula wakati wa Ramadhani.

Mapema, Alhaj Dkt. Mwinyi alijumuika na waumini wa dini ya Kiislamu katika ibada ya Sala ya Ijumaa iliyosaliwa katika Msikiti huo.

Naye Khatibu wa Msikiti huo, Sheikh Khamis Shaaban, amewanasihi waumini wa dini ya Kiislamu kusameheana pale walipokoseana na kuishi kwa kumcha Mwenyezi Mungu.

Ijitimai hiyo ya Kimataifa imehudhuriwa na masheikh pamoja na waumini wa dini ya Kiislamu kutoka nchi mbalimbali za Afrika Mashariki na Kati.

NA MWANDISHI WETU

Bajeti mpya Zanzibar kufikia Sh8.217 trilioni

Kwa mwaka wa fedha 2026/27, Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) inakadiriwa kufikia Sh8.217 trilioni ikiwa ni ongezeko la Sh1.235 trilioni.

Ongezeko hilo ni sawa na ukuaji wa asilimia 17.69 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2025/26 ya Sh6.982 trilioni.

Makadirio hayo yanatokana na mageuzi ya sera na mikakati mbalimbali ya upatikanaji wa mapato ambayo Serikali inapanga kutekeleza kwa mwaka wa fedha 2026/27.

Hayo yalibainishwa jana na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk Malik Akil wakati akiwasilisha mpango wa Taifa na mwelekeo wa bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2026/27 katika mkutano wa 11 wa Baraza la Wawakilishi Chukwani Zanzibar.

Kwa mwaka wa fedha 2026/27, matarajio ya kiwango cha utegemezi wa Bajeti ya SMZ ni kupungua kutoka asilimia 4.9 iliyoripotiwa mwaka 2025/26 hadi kufikia asilimia 4.5 kwa mwaka wa fedha 2026/27.

Kupungua huko kunatokana na mkakati wa Serikali wa kuimarisha ukusanyaji wa mapato na mikopo ya ndani.

Dk Malik alisema katika mpango huo, mapato ya ndani yanakadiriwa kufikia Sh6.613 trilioni ikiwa ni ongezeko la Sh1.076 trilioni sawa na ukuaji wa asilimia 19.4 ikilinganishwa na makadirio ya mwaka 2025/26 ya Sh5.537 trilioni.

Mapato ya ndani yanajumuisha mapato ya kodi na yasiyokuwa ya kodi, mikopo ya ndani na mapato ya mamlaka za Serikali za mitaa na mapato ya taasisi zinazojitegemea.

"Katika mchanganuo huo, Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) itakusanya Sh1.684 trilioni. Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) upande wa Zanzibar Sh1.128 trilioni na mapato ya kodi za wafanyakazi kutoka SMT (Paye) walioko Zanzibar ni Sh21 bilioni," alisema Dk Malik.

Katika makadirio hayo, alisema mapato yasiyokuwa ya kodi yatachangia Sh350.664 bilioni, mikopo ya ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ni Sh2.9 trilioni, mapato ya mamlaka za Serikali za mitaa Sh23.915 bilioni na mapato ya taasisi zinazojitegemea za Serikali Sh505.272 bilioni.

Katika kuhakikisha mapato ya ndani yanaongezeka kwa mwaka 2026/27, alisema Serikali imeandaa mikakati mahsusi ikiwa ni kuongeza kiwango cha fedha kuweka katika mfuko wa kuhudumia madeni ili kuongeza hadhi ya kukopesheka na kuboresha mifumo ya ukusanyaji na kuhakikisha hakuna mapato yatakayokusanywa nje ya mifumo.



Waziri wa Fedha na Mipango wa Zanzibar, Dk Malik Akil akiwasilisha mpango wa Taifa na mwelekeo wa bajeti wa mwaka 2026/27 katika mkutano wa Baraza la Wawakilishi, Unguja jana.

Katika mapato yatokanayo na misaada na mikopo kutoka kwa washirika wa maendeleo yanakadiriwa kufika Sh1.604 trilioni ikiwamo mikopo ya Sh1.062 trilioni na misaada Sh391.750 bilioni, Sh560 bilioni zinazotokana na Mfuko wa Pamoja wa Washirika wa Maendeleo na Sh150 bilioni ni misaada ya kibajeti.

Katika matumizi ya Sh8.217 trilioni, matumizi ya kazi za kawaida inakadiriwa kuwa Sh2.923 trilioni sawa na asilimia 35.58 ya makadirio ya bajeti yote inayojumuisha Sh1.003 trilioni ikiwa ni matumizi ya mshahara.

"Sh698.871 bilioni zitatumika kuendeshea ofisi, Sh701.012 bilioni, matumizi ya huduma za Mfuko Mkuu wa Serikali, Sh14.700 bilioni matumizi ya Serikali za mitaa kwa mapato ya ndani," alisema Dk Malik.

Kwa matumizi ya kazi za maendeleo, alisema Sh5.294 trilioni zinakadiriwa kutumika kwa utekelezaji wa mpango wa maendeleo sawa na asilimia 64.42 ya bajeti yote, zikiwamo Sh2.705 trilioni za matumizi ya miradi mipya ya kimkakati inayoendelea kutoka serikalini na Sh600 bilioni kwa ajili ya mfuko wa kugharamia madeni na Sh542.780 bilioni kwa ajili ya miradi mingine.

Alisema Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango itaendelea na jukumu lake la msingi la utafutaji wa rasilimali fedha ili kugharamia mpango mkakati wa Serikali hususan miradi inayochochea kasi ya ukuaji wa uchumi na kuhakikisha uhimilivu wa deni la Serikali unaendelea kwa kiwango kinachokubalika.

Dk Malik alitaja miongoni mwa hatua ambazo Serikali inakusudia kuziwekea mikakati ni pamoja na usimamizi wa mapato kwa kuimarisha matumizi ya mifumo ya kidijitali, kudhibiti mianya ya ukwepaji kodi, kurahisisha taratibu za kodi, kutoa elimu kwa walipa kodi na kuimarisha ukaguzi wa mapato.

"Pia, kuongeza mapato yasiyo ya kodi kwa kuimarisha usimamizi wa mali za Serikali na ufanisi wa mashirika ya umma ili kuongeza wigo wa mapato ya Serikali yanayotokana na gawio na mchango kutoka kwa taasisi zinazojitegemea," alisema Dk Malik.

MWANDISHI WETU

UN: Tanzania ina mifumo imara ya maridhiano

Rais Samia Suluhu Hassan, amekutana na kufanya mazungumzo na Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Amina Mohammed, ambaye ameisifu Tanzania kwa uimarishaji mifumo ya utatuzi wa changamoto kwa mazungumzo na maridhiano.

Kikao hicho ni mwendelezo wa vikao ambavyo Samia na wasaidizi wake wamekuwa wakivifanya na viongozi mbalimbali wa jumuiya za kikanda na kimataifa, kuimarisha uhusiano na ushirikiano wa kimataifa.

Pia Serikali ya Tanzania kupitia Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Mahmoud Thabit Kombo ameshakutana na Katibu Mkuu wa UN, Antonio Guterres.

Taarifa ya kikao hicho, imetolewa jana na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais Ikulu, Bakari Machumu, kuwa wawili hao wamekutana jijini Addis Ababa, Ethiopia walikokwenda kushiriki mkutano wa wakuu wa nchi wa Umoja wa Afrika (AU).

Katika kikao hicho, Amina aliisifu Tanzania kwa kuimarisha mifumo ya taasisi na utatuzi wa changamoto kwa njia ya mazungumzo na maridhiano.

> "Napongeza na kuthamini mchango wa UN na taasisi zake katika jitihada za pamoja za maendeleo nchini, hususan katika nyanja za ushirikiano wa kidiplomasia na msaada wa maendeleo katika sekta mbalimbali."
>
> **Rais Samia**

Mazungumzo hayo pia, yamegusia mageuzi ya mfumo wa Umoja wa Mataifa, ushiriki wa vijana katika maendeleo na umuhimu wa kuimarisha uratibu kati ya UN na AU.

Kwa upande wa Rais Samia, alieleza dhamira ya Tanzania kuendelea kutekeleza mageuzi ya kiuchumi, kiutawala na kuimarisha ushirikiano wa nchi na UN katika utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs). Alisema mageuzi hayo ni katika sekta zinazogusa maisha ya wananchi wengi ikiwemo afya, elimu, maji safi, usafi wa mazingira, na kupunguza umasikini.

Samia alionesha utayari wa Serikali kumpokea mjumbe maalumu wa UN aliyeomba kuja nchini kwa ajili ya kuwasilisha ujumbe maalumu wa Katibu Mkuu wa UN, António Guterres.

Katika hatua nyingine Februari 13 mwaka huu Rais Samia alifanya mazungumzo na viongozi mbalimbali akiwemo Rais wa Angola, João Lourenço, aliyekubali kufanya ziara ya kiserikali Tanzania na kuwa mgeni rasmi katika Maonesho ya Biashara ya Kimataifa, maarufu Sabasaba mwaka 2026. Pia walisisitiza kuimarisha mahusiano ya kihistoria na ushirikiano wa kimkakati kwa manufaa ya maendeleo ya kiuchumi na ustawi wa wananchi wa pande zote.

Februari 14, mwaka huu Rais Samia alikutana na kuzungumza na Waziri Mkuu wa Ethiopia, Dk Abiy Ahmed, kabla ya ufunguzi rasmi wa Mkutano Mkuu wa Umoja wa Afrika, uliojadili kuimarisha uhusiano wa kidiplomasia, kukuza biashara na uwekezaji.

MWANDISHI WETU

Samia awataka viongozi Afrika kudhibiti malaria

Rais Samia Suluhu Hassan amesema mapambano dhidi ya ugonjwa wa malaria barani Afrika yanahitaji uongozi na usimamizi thabiti wa Waafrika wenyewe, umiliki wa kweli wa programu zake pamoja na dhamira ya kisiasa ya muda mrefu.

Amesema vita dhidi ya malaria si suala la afya pekee, bali ni ajenda ya maendeleo, uchumi na ustawi wa rasilimali watu barani Afrika.

Alitoa kauli hiyo jana, wakati akishiriki katika mkutano wa ngazi ya juu na vyombo vya habari uliolenga kujadili ufadhili endelevu wa mapambano dhidi ya malaria barani Afrika, pembezoni mwa mkutano wa 39 wa wakuu wa nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika (AU) unaofanyika makao makuu ya Umoja huo, jijini Addis Ababa, Ethiopia.

Rais Samia alisema vita dhidi ya malaria si suala la afya pekee, bali ni ajenda ya maendeleo, uchumi na ustawi wa rasilimali watu barani Afrika.

"Mapambano dhidi ya malaria barani Afrika yanahitaji uongozi na usimamizi thabiti wa Waafrika wenyewe, umiliki wa kweli wa programu zake na dhamira ya kisiasa ya muda mrefu," alisema.

Akieleza uzoefu wa nchi katika mapambano dhidi ya malaria, Rais Samia alisema Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazoongoza katika ajenda ya kutokomeza malaria.

Hiyo ni pamoja na kuwa mwenyeji wa African Leaders Malaria Alliance (ALMA) kama taasisi ya kuratibu mapambano hayo barani Afrika, iliyojengwa juu ya mifumo madhubuti ya uwajibikaji, pamoja na uwezo wa utekelezaji unaolenga matokeo.

ALMA ni muungano wa wakuu wa nchi wa Afrika unaolenga kuharakisha kutokomeza malaria na kuimarisha mifumo ya afya.

"Tanzania imewekeza kwa kiasi kikubwa katika tafiti za kisayansi na ubunifu kupitia Taasisi ya Afya Ifakara (IHI), ikiwemo utafiti wa teknolojia za kisasa za kudhibiti maambukizi ya malaria," alisema.

Alibainisha jitihada za Tanzania za kuongeza matumizi ya vyandarua vya kujikinga dhidi ya mbu wanaoeneza malaria, chanjo za malaria, pamoja na kuboresha mifumo ya matibabu na ufuatiliaji wa wagonjwa kama

Rais Samia Suluhu Hassan akishiriki mkutano wa wakuu wa nchi wa Umoja wa Afrika (AU), unafanyika makao makuu ya umoja huo jijini Addis Ababa nchini Ethiopia, jana. Picha na Ikulu

miongoni mwa njia zilizotumika.

"Serikali imeimarisha ushirikiano wa sekta mbalimbali ili kuhakikisha afua za malaria zinaunganishwa kikamilifu katika mfumo wa huduma za afya ya msingi na Mpango wa Bima ya Afya kwa Wote, kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa huduma na kupunguza vifo vitokanavyo na ugonjwa huo," alisema.

Katika kuimarisha ufadhili wa ndani, Rais Samia alisema kupitia mabaraza ya kutokomeza malaria ya Tanzania Bara na Zanzibar, Serikali imeendelea kushirikiana na sekta binafsi, taasisi za dini, asasi za kiraia na wadau wa maendeleo kwenye uhamasishaji wa rasilimali za ndani kwa ajili ya mapambano dhidi ya malaria.

Alitumia nafasi hiyo kusisitiza umuhimu wa ushirikiano wa kimataifa, akieleza kuwa pamoja na jitihada za ndani, taasisi za kimataifa na washirika wa maendeleo wanapaswa kutekeleza ahadi zao kikamilifu na kwa wakati, husuan katika kuimarisha Mfuko wa Dunia wa Kupambana na Malaria (The Global Fund) pamoja na matumizi ya rasilimali za Benki ya Dunia kwa ajili ya programu za malaria.

Kwa upande wake, Rais wa Botswana na Mwenyekiti wa ALMA, Duma Gideon Boko, alisema kwa mujibu wa Ripoti ya Maendeleo ya Malaria Barani Afrika ya mwaka 2025, Afrika bado ipo mbali kufikia lengo la kutokomeza malaria ifikapo mwaka 2030.

Ripoti hiyo ya maendeleo ya malaria Afrika 2025 inaonesha kuwa Afrika bado inabeba zaidi ya asilimia 90 ya maambukizi na vifo vya malaria duniani, huku kasi ya kutokomeza ikipungua.

"Nazihimiza nchi wanachama kutenga bajeti mahsusi kwa ajili ya mapambano dhidi ya malaria, kuanzisha mabaraza ya kutokomeza malaria, pamoja na kutumia mifumo ya takwimu ili kuboresha utekelezaji," alisema.

Naye Kamishna wa Afya, Masuala ya Binadamu na Maendeleo ya Jamii wa AU, Balozi Amma Iwum-Amoah, alisema kupungua kwa ufadhili wa kimataifa katika miaka ya karibuni kumeathiri juhudi za nchi mbalimbali za kupambana na malaria.



MAONI HURU

SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323

Tuache fikra potofu kwamba ghorofani masokoni hakuna wateja

Siku ya tarehe 8 Februari 2026, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alizindua na kulifungua upya Soko Kuu la Kariakoo baada ya soko la awali kukumbwa na janga la kuteketea kwa moto. Uzinduzi huu ulikuwa ishara ya dhamira ya dhati ya Serikali katika kuboresha miundombinu ya biashara na kuendana na kasi ya ukuaji wa miji ya kisasa.

Pamoja na juhudi hizi kubwa, bado tunakabiliwa na changamoto ya mazoea na mitazamo hasi ya jamii, hususan wafanyabiashara na wanunuzi. Watanzania wengi wamezoea kununua na kuuza bidhaa kwenye magenge na masoko ya chini yasiyo ya ghorofa. Mazoea haya yamekuwa kikwazo kikubwa katika matumizi kamili ya masoko ya kisasa.

Wateja wengi huona usumbufu kupanda ngazi au kutumia lifti kwenda kununua bidhaa zilizopo kwenye tabaka za juu. Hali hii imewaathiri wachuuzi walioko juu, kwani hukosa wateja na mitaji yao kudorora. Ndipo imani potofu hujengeka kwamba "wateja wapo chini" na riziki haipatikani juu.

Mtazamo huu unapingana na mafundisho ya dini ya Kiislamu. Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) amesema kwenye Mu'jamu Al-A'rabiy 2/730: "Lau kama mmoja wenu angeikimbia riziki yake, basi ingemfuata kama vile kifo kinavyomfuata." Hii inaonesha wazi kuwa riziki haifungwi na mahali, bali humfuata mwenyewe haki yake.

Zaidi ya hapo, Qur'an inatukumbusha kwa uwazi kabisa: "Na hapana kiumbe chochote kinachotembea juu ya ardhi ila riziki yake iko kwa Mwenyezi Mungu..." [Qur'an, 11: 6]. Aya hii inabomoa kabisa dhana kwamba riziki ipo sehemu fulani tu; chini, kwenye kingo za barabara, au kwenye msongamano wa watu.

Changamoto kubwa tuliyonayo leo si uhaba wa masoko, bali ni uhaba wa uelewa na kukosa imani sahihi kuhusu riziki. Wachuuzi wengi wanasahau kuwa riziki huandikwa na Mwenyezi Mungu, na hupatikana kwa kuchukua sababu halali na kuamini popote mtu alipo riziki itamfikia.

Ndiyo maana Mtume Muhammad kwenye Muwattwau wa Imam Malik 5/1326 alisisitiza maadili katika kutafuta riziki aliposema kuwa hakuna nafsi itakayokufa mpaka ikamilishiwe riziki yake, na akaelekeza tutafute kwa njia nzuri, kwani kilicho kwa Mwenyezi Mungu hupatikana kwa kumtii."

Hivyo basi, ni wajibu wetu kubadili fikra. Masoko na maduka ya ghorofani si kuleta usumbufu, bali ni fursa. Riziki inaweza kupatikana chini au juu, mradi mfanyabiashara awe na bidhaa bora, mazingira safi, huduma nzuri na maadili mema.

Wasimamizi wa masoko nao wana mchango mkubwa katika kurekebisha mitazamo hii. Kama aina fulani za bidhaa zinapatikana huko juu tu na hakuna ruhusa ya kuuzwa chini, bila shaka hata wale wavivu wa kupanda ngazi wataenda tu huko.

Kwa sababu ukweli unabaki palepale: Mazoea yana tabu, lakini riziki iliyoandikwa itakufuata popote ulipo.

Mazoea ni tabu, mabadiliko ni lazima

MAKALA YA AFYA

0764 101 018

DKT.
Omar A. Kasuwi
Daktari Bingwa Mshauri wa magonjwa Moyo!
Hospitali ya Chuo Kikuu cha Sokoine (SUA)

Faida ya amadhani (Swawm) kwa msingi wa sayansi na Uisilamu wenyewe.!

Fasting ama kufunga mwezi wa Ramadhani ni ibada inayofanywa na mamilioni ya Waislamu duniani kila mwaka. Kuanzia alfajiri hadi jua kuzama hakuna chakula wala kinywaji kinachotumika kwa muda wa siku 29-30.Baada ya magharibi, kula huruhusiwa kwa muda maalum wa usiku.Kwa mtazamo wa kidaktari, mpangilio huu unafanana sana na tiba ya kisasa inayoitwa kula kwa muda maalum (time-restricted eating)kulingana na saa ya mwili- circadian rhythm.

Kwa maneno rahisi,mwili hupata muda wa kula, na muda wa kupumzika na kujirekebisha.Ni muhimu kuelewa,kuwa kufunga si njaa inayodhuru mwili. Ni hali ya kiasili ambayo mwili wa binadamu umeumbwa kuimudu na hata kunufaika nayo nyakati za dharura. Kinachoifanya Ramadhani kuwa maalum, ni muunganiko wa mabadiliko ya mwili na mafunzo ya makusudi ya nafsi — mwili hubadilika huku akili ikifundishwa nidhamu.

Allah anasema katika Qur'an:

“Enyi mlioamini, mmefaradhishwa kufunga kama walivyofaradhishwa waliokuwa kabla yenu ili mpate kumcha Mungu (Taqwa).”

(Qur'an 2:183)-Hivyo lengo kuu ni uchamungu, lakini wakati huo huo mwili hupitia mabadiliko muhimu yanayopimika kisayansi.

Mabadiliko muhimu yanayotokea



mwilini Wakati wa Kufunga :-!

Mabadiliko ya Nishati :-Mwili Hubadilisha Mafuta kuwa Chanzo Kikuu cha kutengeneza nguvu(metabolic switch)

Masaa kadhaa baada ya kula daku, wingi wa sukari iliyoko katika damu ya hupungua na mwili kupitia homoni maalumu huanza kutumia akiba ya glycogen kutoka kwenye ini. Baada ya takribani nusu ya siku, mwili hubadilisha tena njia ya kutengeneza nguvu kupitia mafuta yaliomwilini.

Mchakato huu huzalisha ketone bodies (nishati safi kwa matumizi ya ubongo). Utafiti unaonyesha kufunga kwa wakati wa Ramadhani husababisha mabadiliko makubwa ya kimetaboliki, ikiwemo matumizi ya glykojeni na mafuta kupata nishati. Hili ni muhimu kwa sababu magonjwa mengi ya kisasa hutokana na kinyume chake — kula mara kwa mara ambako hupelekea homoni ya insulin kuwa juu wakati wote.

Hii inatufundisha jinsi Allah alivyomuumba mwanadamu, na kumuekea njia za mwili kujifunza kutumia nishati kwa ufanisi bila kutegemea kula mara kwa mara hali hii humsaidia mwanadamu hata katika nyakati mbali mbali za dharura, katika maisha yake .

Mtume alisema:

“Mwanaadamu hajajaza chombo kibaya zaidi kuliko tumbo lake. Inamtosha kula vijisehemu vinavyomnyoosha mgongo.”

(Tirmidhi).

Kurekebika kwa Insulini na Kinga Dhidi ya Kisukari!

Katika maisha ya kawaida, kula mara nyingi huifanya hooni ya insulini ibaki juu siku nzima.

Insulini ya juu husababisha kuhifadhi mafuta mwilini na hatimaye usugu wa vipokeo vya “insulin” receptors. Kufunga Ramadhani hupunguza muda ambao insulini iko juu na kuboresha mwitikio wa seli za mwili kwa sukari.Tafiti nyingi zinaonyesha kufunga Ramadhani mara zote huboresha uwezo wa mwili kutumia insulini, hupunguza sukari inayoingia kwenye mzunguko wa damu , huondoa usugu wa resepta za isuline na hivo hupunguza hatari ya magonjwa ya kimetaboliki” (metabolic syndrome”)kama uzito wa ziada ,kisukari nk.

Kuimarika kwa Afya ya Moyo na Mishipa ya Damu!

Hatari za Moyo hupungua wakati wa Ramadhani ikiwa ulaji ni wa kiasi. Tafiti nyingi duniani zinaonyesha kupungua kwa LDL (cholesterol mbaya), kupungu triglycerides, kuongezekaHDL (cholesterol nzuri) Kupungua kwa shinikizo la juu la damu na kuboreshwa kwa mzunguko mzima wa damu mwilini. Kwa pamoja hupunguza hatari ya muda mrefu ya magonjwa ya moyo.

Mabadiliko ya mwili siku za mwanzo za kuanza Kufunga ,watu huisi kichwa kuuma, mwili kuwa mdhaifu na baadhi huwa ni wenye kupatwa na hasira mara kwa mara .Hali hii haina maana ya mwili kuondoa Sumu mwilini kama ambavyo imezoeleka na watu wengi bali ni hali ya mwili kuanza kuzoea sukari kidogo, hali ya kupungua kwa Cafein mwilini kwa waliozoea kutumia kiasi kingi cha kafeini, na mapungufu ya maji mwilini, kwa ujumla ni mabadiliko ya kikemikali kutokana na hali hiyo ya kufunga.

Itaendelea toleo lijalo

NA MWANDISHI WETU

Ramadhan ya tatu mfululizo Wapalestina wangali katika mateso

Mwaka wa tatu wa vita unapoanza kuhesabiwa, Wapalestina wanaikaribisha Ramadhan ya tatu mfululizo wakiwa katika hali ya mateso, huzuni na majonzi yasiyo na mfano.

Katika ardhi ya Palestina, hususan Ukanda wa Gaza, Mwezi Mtukufu unaingia huku sauti za mabomu zikichanganyika na adhana za Magharibi, na taa za misikiti zikichomoza katikati ya vifusi vya majengo yaliyobomolewa.

Ramadhan, ambayo kwa Waislamu ni mwezi wa rehema, subira na mshikamano, kwa Wapalestina wengi umegeuka kuwa mwezi wa majaribu makubwa chini ya kile wanachokiona kama uvamizi na uonevu wa muda mrefu wa dola ya Israel.

Katika muktadha wa Kiislamu, Palestina ni ardhi yenye utakatifu maalum. Ndani yake mmo mji wa Al-Quds, unaohifadhi Msikiti wa Al-Aqsa, Qibla ya kwanza ya Waislamu na eneo la tukio la Israa na Mi'raj ya Mtume Muhammad (rehema za Allah na amani zimshukie).

Hivyo basi, kwa mamilioni ya Waislamu duniani, kuzingirwa kwa Gaza, vizuizi katika Ukingo wa Magharibi na mashambulizi yanayoripotiwa karibu na maeneo matakatifu, vinafasiriwa kama siasa za kimabavu zinazolenga kudhibiti si tu ardhi bali pia utambulisho na imani ya Kiislamu.

Licha ya makubaliano ya kusitisha mapigano, hali ya sasa inaonesha mzunguko wa ghasia usioisha: mashambulizi ya kijeshi, makombora, vifo vya raia na uharibifu wa miundombinu ya msingi kama hospitali, shule na misikiti.

Katika Ramadhan, ambapo Waislamu hukusanyika kwa futari na swala za Tarawehe, familia nyingi za Kipalestina zinatekeleza, swaumu bila uhakika wa chakula cha kutosha, maji safi au umeme.

Mifumo ya misaada ya kibinadamu imekuwa ikikumbwa na vikwazo, huku idadi ya waliokimbia makazi yao ikiongezeka. Hii si tu simulizi ya vita bali ni taswira ya mgogoro wa kibinadamu unaogusa misingi ya utu.

Kwa mtazamo wa kisheria na kisiasa, jumuiya ya kimataifa imekuwa ikitoa matamko ya kulaani au kuitaka pande zote kujizuia, lakini kwa wengi katika ulimwengu wa Kiislamu, hatua hizo ni dhaifu au zenye upendeleo. Wazo la "usalama wa Israel" limekuwa likipewa uzito mkubwa katika majukwaa ya kimataifa, wakati madai ya Wapalestina ya haki ya kuishi kwa amani na kujitawala yakionekana kusukumwa pembeni.

Hali hii imezalisha hisia za kukata tamaa, hasira na maumivu katika mioyo ya Waislamu wengi wanaoona mizani ya haki ikiegemea upande mmoja. Ramadhan, hata hivyo, hubeba funzo la subira (sabr) na matumaini (raja). Katika historia ya Uislamu, vipindi vya dhiki vimekuwa pia vipindi vya kujijenga kiimani na kijamii. Maoni huria yanaweza kuuliza: Je, dunia itavumilia kwa muda gani hali hii iendelee? Je, mazungumzo ya amani yatarejeshwa kwa dhati, au vita vitaendelea kuwa mzunguko usiokatika?

Wakati mataifa makubwa yakipima maslahi yao ya kijiografia na kisiasa, maisha ya watoto, wanawake na wazee wa Palestina yanaendelea kuathirika kila siku.

MAHMOUD NYAMGUMA

Israel kudhibiti Waislamu kuingia Masjid Aqsa Ramadhan hii

Siku chache kabla ya kuufikia mwezi wa Ramadhan, Mamlaka za Israel zinapanga kuweka vikwazo vipya vya kuzuia au kupunguza idadi ya Waislamu wanaoruhusiwa kuingia katika Msikiti wa Al-Aqsa wakati wa mwezi mtukufu wa Ramadhan.

Hatua hiyo imelalamikiwa vikali na viongozi wa Kiislamu kuwa ni kinyume cha uhuru wa kuabudu.

Sheikh Ekrima Sabri, Mufti Mkuu wa zamani wa Al Quds na Mkuu wa Baraza Kuu la Kiislamu, amesema hatua hizo zitapunguza kwa kiasi kikubwa idadi ya Waumini wanaoswali katika eneo hilo takatifu, la tatu kwa utakatifu katika Uislamu.

Kwa mujibu wa takwimu za Idara ya Waqf ya Kiislamu, katika miaka ya kawaida zaidi ya Waumini 200,000 hukusanyika kuswali Ijumaa za Ramadhan ndani ya eneo la Al-Aqsa, huku mamia ya maelfu kutoka Ukingo wa Magharibi wakisafiri hadi Al Quds Mashariki.

Hata hivyo, tangu kuanza kwa vita Oktoba 7, 2023, vizuizi vya kijeshi na masharti ya vibali yameimarishwa ili kuruhusu idadi ndogo tu ya Wapalestina kuvuka vituo vya ukaguzi, hali ambayo utekelezaji wa ibada kuwa mgumu zaidi.

Haaretz limeripoti kuwa hatua hizo zinaenda sambamba na ajenda za wanasiasa wa mrengo mkali serikalini, huku uteuzi wa Meja Jenerali Avshalom Peled kama kamanda mpya wa polisi huko Jerusalem Mashariki ukitafsiriwa na wachambuzi kama ishara ya kuimarishwa kwa udhibiti katika eneo la Al-Aqsa.

Sheikh Sabri amesema makumi ya vijana tayari wamepigwa marufuku kuingia msikitini kwa amri za muda zinazodumu hadi miezi sita, akionya kuwa "hii ni kinyume cha mila na uhuru wa kuabudu."

Serikali ya Israel, inayoongozwa na Waziri Mkuu Benjamin Netanyahu, imekuwa ikikanusha madai ya kubadili utaratibu wa kihistoria wa eneo hilo, ikisema hatua za kiusalama ni muhimu kulinda utulivu. Israel kuruhusiwa makundi ya wenye misimamo mikali kuingia katika eneo la msikiti tangu 2003, licha ya pingamizi za Waqf, kumezidisha taharuki na kuamsha hofu ya kuingiliwa kwa mamlaka ya Kiislamu.

Sheikh Sabri alitoa wito kwa Jumuiya za Kiarabu na Kiislamu kuonesha mshikamano na Wapalestina wa Al Quds katika kipindi hiki cha Ramadhan, akisisitiza kuwa kuulinda msikiti wa Al-Aqsa ni jukumu la pamoja la Umma wa Kiislamu.



Tamasha la Makka Halal Forum 2026 lanoga

Jukwaa la tatu la Makka Halal Forum 2026 limemalizika jijini Makka, Saudi Arabia, chini ya kaulimbiu "Halal: A Professional Industry" likilenga kuimarisha sekta ya halal duniani kupitia ushirikiano kati ya taasisi za serikali, sekta binafsi na mashirika ya ndani na nje ya nchi.

Kongamano hilo lililoanza Februari 14 hadi 16 katika Kituo cha Maonesho na Matukio cha Chama cha Biashara Makka limedhaminiwa na Waziri wa Biashara wa Saudi Arabia, Dkt. Majid bin Abdullah Al-Kassabi.

Toleo la mwaka huu limevutia ushiriki mpana wa kimataifa kutoka miongoni mwa viongozi, wataalamu na watunga sera kutoka zaidi ya nchi 16,

Sekta ya halal inaendelea kukua kwa kasi, huku matumizi ya Waislamu duniani yakifikia dola trilioni 2.42 mwaka 2023 na kutarajiwa kufikia trilioni 3.36 ifikapo 2028. Jukwaa hilo linaendana na Dira ya 2030 ya Saudi Arabia ya kuimarisha nafasi yake katika uchumi wa halal duniani.

Mashirika 1,800 ya uratibu wa Umra yasitishiwa mikataba

Serikali ya Saudi Arabia imesitisha mikataba ya zaidi ya mashirika 1,800 ya kigeni yanayoratibu safari za Umra kufuatia ukaguzi uliobaini udhaifu katika utoaji wa huduma na kutokuzingatia viwango vilivyowekwa.

Uamuzi huo ulitangazwa Februari 2026 na Wizara ya Hija na Umrah, ikiwa ni sehemu ya juhudi za kulinda haki za mahujaji na kuboresha ubora wa huduma.

Mashirika yaliyosimamishwa yanawakilisha karibu theluthi moja ya mashirika 5,800 yaliyokuwa yakifanya kazi katika sekta hiyo. Hata hivyo, wizara imeeleza kuwa hatua hiyo inahusu utoaji wa visa mpya pekee, huku mahujaji ambao tayari wana visa halali au uhifadhi wa huduma wakiendelea kuhudumiwa kama ilivyopangwa. Mashirika husika yamepewa muda wa siku 10 kurekebisha kasoro na kukidhi viwango vinavyotakiwa ili kurejeshewa mikataba yao.

Wizara imesisitiza kuwa lengo kuu ni kuhakikisha huduma za uhakika, malazi bora na usafiri unaoratibiwa ipasavyo kwa mahujaji wanaozuru Makka na Madina. Hatua hii inaonyesha dhamira ya Saudi Arabia ya kuinua sekta ya utalii wa kidini, hasa wakati idadi ya mahujaji wa kimataifa ikiendelea kuongezeka kila mwaka.

Vyeti vya Halal vyafungua soko la kimataifa kwa bidhaa za Vietnam

Vyeti vya halal vinaendelea kugeuka kuwa daraja muhimu linalofungua milango kwa bidhaa za Vietnam kuingia kwa kasi katika soko la kimataifa la Waislamu.

Kadiri nchi hiyo inavyopanga upya masoko yake ya mauzo ya nje ili kupanua wigo na kupunguza utegemezi kwa washirika wa jadi, soko la halal linaonekana kuwa fursa mpya ya ukuaji endelevu.

Takwimu za taasisi za kimataifa zinaonyesha idadi ya Waislamu duniani imevuka bilioni mbili, ikiwa ni takribani robo ya watu wote duniani. Uchumi wa halal nao unakadiriwa kufikia karibu dola trilioni 5 ifikapo 2030, ukihusisha chakula, vipodozi, dawa, usafirishaji, utalii na hata fedha za Kiislamu.

Hata wasiokuwa Waislamu wanazidi kuvutiwa na bidhaa zenye nembo ya halal kwa sababu huonekana kuwa alama ya ubora, usalama na ufuatiliaji wa uzalishaji.

Kampuni ya HR Essence ni mfano: baada ya kupata cheti kupitia Kituo cha Taifa cha Uthibitishaji Halal, ilisafirisha mzigo wake wa kwanza Malaysia—soko lenye viwango vikali.

Wataalamu wanasisitiza kuwa halal si "tiketi ya kuuza nje" tu; ni mkakati wa muda mrefu unaolazimisha kuboresha mnyororo mzima wa thamani, utawala wa ubora, chapa na mawasiliano yanayoendana na utamaduni wa walaji wa Kiislamu.

Saudi Arabia yatabiriwa kuongoza ukuaji wa Fedha za Kiislamu duniani

Saudi Arabia inatarajiwa kuongoza wimbi jipya la ukuaji wa sekta ya fedha za Kiislamu duniani, huku soko la kimataifa likikadiriwa kukua kutoka dola bilioni 3.7 mwaka 2025 hadi dola bilioni 7.4 ifikapo 2033, kwa mujibu wa utafiti wa Straits Research.

Akizungumza katika kongamano la sekta binafsi lililoandaliwa na Mfuko wa Uwekezaji wa Umma (PIF) jijini Riyadh, mwanzilishi wa Blue Five Capital, Hazem Ben-Gacem, alisema Saudi Arabia ina nafasi ya kipekee kuongoza mwelekeo wa udhibiti na ubunifu wa bidhaa za kifedha zinazozingatia Sharia.

Fedha za Kiislamu zinakataza riba na kuhimiza mgawanyo wa faida na hasara kupitia mikataba kama mudarabah na musharakah. Nchini Saudi Arabia, takribani asilimia 85 ya miamala yote inazingatia misingi ya Sharia, kiwango cha juu zaidi duniani katika masoko yenye mchanganyiko wa benki za kawaida na za Kiislamu, kwa mujibu wa Fitch Ratings.

Benki zote kuu za Saudi Arabia hutoa huduma za Kiislamu, huku Al Rajhi Bank na Alinma Bank zikiwa benki kamili za Kiislamu. Sekta hiyo pia ni mhimili muhimu wa Dira ya 2030, hasa katika kufadhili miradi ya miundombinu, makazi na utalii kupitia mifumo kama murabaha na sukuk.

Indonesia yalenga kuwa kitovu cha kimataifa cha Halal ifikapo 2029

Indonesia imeweka lengo la kuwa kitovu cha kimataifa cha tasnia ya halal ifikapo 2029, ikitumia nafasi yake kama nchi yenye idadi kubwa zaidi ya Waislamu duniani.

Hata hivyo, maofisa wa serikali wameonya kuwa taifa hilo “linachelewa” na lazima liongeze kasi ya ujenzi wa uwezo wa utoaji vyeti, miundombinu na huduma za ufadhili unaozingatia Sharia ili kushindana na vinara kama Malaysia na Saudi Arabia.

Naibu mwenyekiti wa Wakala wa Dhamana ya Bidhaa Halal (BPJPH), Chuzaemi Abidin, amesema Indonesia ilianza kuchelewa licha ya kuwa na soko kubwa, ikizingatia kwamba sheria ya uthibitishaji halal ilipitishwa mwaka 2014 na BPJPH kuwa wakala huru mwishoni mwa 2024.

Kwa sasa, takribani biashara milioni 3 pekee ndizo zimepata uthibitisho wa halal kati ya takriban MSMEs milioni 64, huku bidhaa milioni 11.5 zikiwa tayari zimethibitishwa. BPJPH imesema bajeti itawezesha kutoa uthibitisho wa bure kwa biashara milioni 1.35 mwaka 2026, wakati waombaji binafsi wakilipa rupiah 230,000.

Dirisha la Kiislamu ruhsa Benki ya viwanda Nigeria

Benki ya Maendeleo ya Viwanda ya Nigeria imepata kibali kutoka Benki Kuu ya Nigeria (CBN) kufungua dirisha la huduma za fedha za Kiislamu, hatua inayolenga kupanua upatikanaji wa mikopo kwa misingi ya Sharia.

Kupitia dirisha hilo, BoI sasa itatoa bidhaa kama Ijara (ukodishaji wa mali) na Mudaraba (ushirikiano wa kugawana faida), ambazo hazihusishi riba bali zinategemea mgawanyo wa hatari na faida kati ya benki na mteja.

Hatua hiyo itaiwezesha benki kufikia wafanyabiashara na wawekezaji wasiopata huduma za kifedha kwa urahisi kupitia mfumo wa kawaida wa kibenki.

Mkurugenzi Mtendaji wa BoI, Olasupo Olusi, alisema uamuzi huo utaimarisha uwezo wa benki kufadhili mali na bidhaa kwa miundo inayozingatia Sharia, huku ukichochea maendeleo jumuishi ya viwanda.

Kwa zaidi ya muongo mmoja, Nigeria imeruhusu benki za Kiislamu, ikiwemo Jaiz Bank, na serikali imekuwa ikitoa sukuk kufadhili miradi ya miundombinu. Hatua ya BoI inaongeza wigo wa fedha za Kiislamu katika sekta halisi ya uchumi.

HABARI
HUDUMA ZA KIFEDHA ZA KIISLAMU

ADIB yatajwa benki bora ya Kiislamu Mashariki ya Kati

Benki ya Abu Dhabi Islamic Bank (ADIB) imetangazwa kuwa Benki Bora ya Kiislamu Mashariki ya Kati na Falme za Kiarabu (UAE) na jarida mashuhuri la masuala ya fedha la EMEA Finance.

Tuzo hiyo inatambua mafanikio makubwa ya benki hiyo katika mwaka 2025, ikiwemo ukuaji imara wa kifedha na ubunifu wa huduma za kibenki zinazozingatia misingi ya Sharia.

Kwa mujibu wa taarifa kwa vyombo vya habari, ADIB ilirekodi ongezeko la mwaka hadi mwaka katika vipimo muhimu vya kifedha, ikiwemo kuimarika kwa faida, ongezeko la amana za wateja na ukuaji wa mikopo ya kifedha.

Mafanikio hayo yalichangiwa na utekelezaji thabiti wa mkakati wake wa biashara, pamoja na kuimarika kwa huduma kwa wateja na upanuzi wa mapato kutoka vyanzo mbalimbali.

Katika mwaka 2025, benki hiyo pia iliharakisha mabadiliko ya kidijitali kwa kuboresha huduma za mtandaoni na simu, kurahisisha ufunguzi wa akaunti na kupunguza muda wa upatikanaji wa huduma. Maboresho hayo yameongeza urahisi kwa wateja binafsi na wa biashara, sambamba na kuimarisha usalama wa miamala ya kifedha.Aidha, ADIB imeendeleza juhudi za uendelevu, ujumuishaji wa kifedha na maendeleo ya rasilimali watu. Benki hiyo imekuwa ikisisitiza utoaji wa huduma jumuishi kwa makundi mbalimbali ya jamii, pamoja na kuwekeza katika mafunzo na maendeleo ya wafanyakazi wake ili kuhakikisha ubora wa huduma unaendana na viwango vya kimataifa.

Kupitia utekelezaji wa Dira ya 2035, ADIB inalenga kukuza ukuaji endelevu na kuimarisha thamani ya muda mrefu kwa wadau wake, wakiwemo wateja, wawekezaji na jamii kwa ujumla. Tuzo hiyo kutoka EMEA Finance inaweka bayana nafasi ya ADIB kama miongoni mwa taasisi zinazoongoza katika sekta ya fedha za Kiislamu katika ukanda wa Mashariki ya Kati.

Mashirika 1,800 ya uratibu wa Umra yasitishiwa mikataba

Serikali ya Saudi Arabia imesitisha mikataba ya zaidi ya mashirika 1,800 ya kigeni yanayoratibu safari za Umra kufuatia ukaguzi uliobaini udhaifu katika utoaji wa huduma na kutokuzingatia viwango vilivyowekwa.

Uamuzi huo ulitangazwa Februari 2026 na Wizara ya Hija na Umrah, ikiwa ni sehemu ya juhudi za kulinda haki za mahujaji na kuboresha ubora wa huduma.

Mashirika yaliyosimamishwa yanawakilisha karibu theluthi moja ya mashirika 5,800 yaliyokuwa yakifanya kazi katika sekta hiyo. Hata hivyo, wizara imeeleza kuwa hatua hiyo inahusu utoaji wa visa mpya pekee, huku mahujaji ambao tayari wana visa halali au uhifadhi wa huduma wakiendelea kuhudumiwa kama ilivyopangwa. Mashirika husika yamepewa muda wa siku 10 kurekebisha kasoro na kukidhi viwango vinavyotakiwa ili kurejeshewa mikataba yao.

Wizara imesisitiza kuwa lengo kuu ni kuhakikisha huduma za uhakika, malazi bora na usafiri unaoratibiwa ipasavyo kwa mahujaji wanaozuru Makka na Madina. Hatua hii inaonyesha dhamira ya Saudi Arabia ya kuinua sekta ya utalii wa kidini, hasa wakati idadi ya mahujaji wa kimataifa ikiendelea kuongezeka kila mwaka.

Vyeti vya Halal vyafungua soko la kimataifa kwa bidhaa za Vietnam

Vyeti vya halal vinaendelea kugeuka kuwa daraja muhimu linalofungua milango kwa bidhaa za Vietnam kuingia kwa kasi katika soko la kimataifa la Waislamu.

Kadiri nchi hiyo inavyopanga upya masoko yake ya mauzo ya nje ili kupanua wigo na kupunguza utegemezi kwa washirika wa jadi, soko la halal linaonekana kuwa fursa mpya ya ukuaji endelevu.

Takwimu za taasisi za kimataifa zinaonyesha idadi ya Waislamu duniani imevuka bilioni mbili, ikiwa ni takribani robo ya watu wote duniani. Uchumi wa halal nao unakadiriwa kufikia karibu dola trilioni 5 ifikapo 2030, ukihusisha chakula, vipodozi, dawa, usafirishaji, utalii na hata fedha za Kiislamu.

Hata wasiokuwa Waislamu wanazidi kuvutiwa na bidhaa zenye nembo ya halal kwa sababu huonekana kuwa alama ya ubora, usalama na ufuatiliaji wa uzalishaji.

Kampuni ya HR Essence ni mfano: baada ya kupata cheti kupitia Kituo cha Taifa cha Uthibitishaji Halal, ilisafirisha mzigo wake wa kwanza Malaysia—soko lenye viwango vikali.

Wataalamu wanasisitiza kuwa halal si "tiketi ya kuuza nje" tu; ni mkakati wa muda mrefu unaolazimisha kuboresha mnyororo mzima wa thamani, utawala wa ubora, chapa na mawasiliano yanayoendana na utamaduni wa walaji wa Kiislamu.

Msamvu, Morogoro
P.O.Box 6011
Morogoro,
Tanzania

Mhariri
+255 789 201383

Hana funga muongo, asiyeacha maovu

Funga ya Ramadhan ni miongoni mwa masomo makuu ya vitendo (practical) ambayo humuandaa mfungaji wa kweli kuwa mchamungu. Funga hii, pia huilea nafsi ya mfungaji na kumkataza kufanya mambo yaliyoharamishwa. Hii ina maana, funga ya Ramadhan ni mazoezi ya kimwili na kiroho ambayo humtayarisha Muislamu kukabiliana na matukio ya ghafla, yenye kuhuzunisha na kutia simanzi.

Kwa hakika, kufunga si kujizuwia kula na kunywa tu. Ni zaidi ya hapo. Ukiacha kujizuwia kula na kunywa, tunapaswa pia kujizuwia na mambo mengine ya maasi ikiwemo kusema uongo, kutukana, kusengenya, kufitinisha au kuchonganisha watu, kucheza kamari, kutazama haramu, na kadhalika.

Mtume (rehema na amani ya Allah imshukie) amesema: "Yeyote ambaye hatoacha kusema uongo, kusengenya, kufitinisha, kutoa ushuhuda wa uongo, basi ajue kuwa Allah hana haja na swaumu yake katika kuacha chakula chake na kinywaji chake." [Bukhari na Muslim].

Ni jambo la kusikitisha kuwa, wapo wanaochuma mali (fedha) kwa njia za haramu, ikiwamo kucheza ama kutangaza matangazo yanayohamasisha kucheza kamari hali ya kuwa wamefunga. Baadhi ya kinamama wanatembea uchi barabarani na kujipamba kwa manukato na mapambo mengine ya haramu wakidhani kutokula na kunywa katika mchana wa Ramadhan kumetosha swaumu zao kukubaliwa na Mwenyezi Mungu. Huko ofisini, watu wanafunga na huku wakijihusisha na ubadhirifu wa mali za umma, kutakatisha fedha na kula rushwa kwa kudhani kuwa kufanya hivyo si dhambi.

Kinachosikitisha zaidi ni kwamba, wengi miongoni mwetu Waislamu tunafunga pasina kusali; na hili ni kosa kubwa kisheria. Juu ya hilo, wanazuoni wengi wa sheria ya Kiislamu (Fuqahaau) wamesema swaumu haikubaliwi pasina kusali. Vilevile, ni makosa makubwa mtu kusali siku za mwanzo wa Ramadhan na kisha kuzembea au kuacha kusali katika siku zilizobaki.

Wapo pia baadhi yetu wanaoitakidi kuwa kuangalia tamthilia na sinema ni halali kisheria.

Ukweli ni kwamba, tamthilia nyingi zina maudhui machafu ndiyo maana sheria inawataka Waislamu kuinamisha chini macho yao wasiangalie mambo ya haramu. Hivyo basi, Ramadhan hii iwe ni fursa adhimu ya kusahihisha makosa haya ili nafsi zetu zibadilike na kuielekea twa'a ya Allah.

Ramadhan ni mwezi wenye fadhila, ubora na kheri nyingi hasa kwa yule mwenye kufunga na kudumisha ibada ya sala, akawa pia ni mwenye kujitahidi kutumia fursa alizopewa na Allah katika kuchuma kheri.

Atakayeafikishwa katika hayo, kwa hakika amefuzu na ametangulia mbele katika kheri; na yule asiyefunga au kufanya uzembe katika kuziendea ibada ndani ya Ramadhan atakuwa amepata hasara. Waislamu tuna haja ya kuwekeza muda wetu katika mambo ya kheri ili tupate radhi za Allah na hatimaye tuingie katika Pepo yake.

Allah Aliyetukuka anasema: "Mwenye kufanya mema – awe mwanaume au mwanamke hali ya kuwa ni Muumini, tutampa uhai ulio mzuri; na tutawalipa (huko Akhera) malipo yao kutokana na mazuri waliyokuwa wakiyafanya." [Qur'an, 16:97].

Hivyo, huu ni muda mwafaka kwa wale wenye kupigania fursa za misimu ya kheri, kuhakikisha kuwa hawatoki mikono mitupu katika msimu huu wa Ramadhan, kwani mja hawezi kufikia daraja ya uchamungu isipokuwa kwa kudumisha matendo mema.

MAKALA
MAALUM

Na Sheikh Seif Ruga
0712 690 811

Zijue adabu na taratibu za kubisha hodi

Hakika Uislamu umeipa nafasi kubwa sana elimu ya malezi ya kijamii. Uislamu haukuacha jambo lolote – liwe dogo au kubwa isipokuwa umelifafanua, umebainisha kwa kina haki za wazazi, wanandoa na watoto, haki za majirani, pamoja na miamala yote na maadili ya Kiislamu.

Zijue adabu na taratibu za kubisha hodi

Hakika Uislamu umeipa nafasi kubwa sana elimu ya malezi ya kijamii. Uislamu haukuacha jambo lolote – liwe dogo au kubwa isipokuwa umelifafanua, umebainisha kwa kina haki za wazazi, wanandoa na watoto, haki za majirani, pamoja na miamala yote na maadili ya Kiislamu.

Miongoni mwa maadili hayo ni adabu ya kupiga hodi. Adabu hii ni jambo nyeti na muhimu linalokuza hisia za kuwajali na kuwaheshimu wengine, na ni alama iliyo wazi miongoni mwa misingi ya malezi ya kijamii.

Allah Mtukufu ameielezea adabu hii kwa kina ndani ya Qur'an Tukufu aliposema: "Enyi mliyoamini! Msiingie nyumba zisizo zenu mpaka mwombe ruhusa, na muwatolee salamu wenyewe. Hayo ni bora kwenu ili mpate kukumbuka." [Qur'an, 24:27].

Hakika tofauti nyingi za uhusiano wetu wa kijamii zinarejea kwenye ukweli kwamba wapo watu wasiofahamu mipaka yao wanapoamiliana na wengine. Hawajui wapi wanapaswa kusimama ili wasivuke mipaka hiyo, wala hawatambui ule 'mstari mwekundu' unaopaswa kuheshimiwa, ili wasiwe mzigo mzito kwa wengine na kuwadhuru katika dini yao, heshima na maisha yao ya kila siku.

Wanazuoni wa sharia ya Kiislamu wamefafanua maana ya kupiga hodi kuwa ni kuomba idhini kwa adabu, kwa lengo la kujiepusha na kuangalia uchi au mambo yasiyopasa kuonekana.

Vilevile, wapo waliosema kuwa ni kuomba ruhusa ya kuingia katika sehemu ambayo si miliki ya anayeomba ruhusa. Mtazamo wa kina juu ya siri na hekima za adabu ya kupiga hodi unaonesha uhalisia wake na busara iliyomo ndani yake.

Mwanadamu ameumbwa na silika ya matamanio na tamaa; na si kila mtu anaweza kuzuia tamaa zake na visababishi vyake kwa msukumo wa dhamira ya kibinadamu au kwa misukumo ya utu na heshima. Badala yake hujizuia zaidi kwa msukumo wa imani.

Sharia ya Kiislamu ina hukumu nyepesi na mtazamo wa mbali ulio wa kina; kwani inapokataza jambo fulani, hukataza pia kila njia na kichocheo kinachopelekea kwenye jambo hilo. Na hapa ndipo penye tofauti kati ya sharia za Allah na zile zilizotungwa na wanadamu.

Kwa mfano, Uislamu ulipokataza zinaa ulikataza pia visababishi vyake kama vile kutazama kwa haramu, kukaa faraghani, kuonesha maungo ya mwili, na kila kinachopelekea katika zinaa.

Kubisha hodi ni adabu ya hali ya juu inayolinda heshima na mipaka ya nyumba. Ikiwa hakuna mtu yeyote wa kutoa ruhusa ya kuingia ndani ya nyumba, basi subiri hadi utakaporuhusiwa. Hii ni kwa sababu, kuomba ruhusa kunahusiana na heshima ya nyumba na wakaazi wake.

Allah Mtukufu anasema: "Na msipokuta humo yeyote, basi msiingie mpaka mruhusiwe. Na mkiambiwa: Rudini! Basi rudini. Huo ni usafi zaidi kwenu. Na Mwenyezi Mungu anajua mnayoyatenda." [Qur'an, 24:28].

Hii inaonesha kwamba mgeni anatakiwa kurudi nyuma katika hali mbili. Mosi, anapokosa ruhusa ya wazi ya kuingia, kama vile kuambiwa 'rudi' au 'usingie'. Pili, anapokosa ruhusa isiyo ya wazi kama hakuna mtu wa kumwitikia hodi yake. Hakika nyumba za Waislamu zina heshima kubwa mno.

Mtume wa Allah (rehema na amani ziwe juu yake) ameilinda heshima hii kwa kuweka adhabu kali kwa anayekiuka: "Lau mtu angechungulia kwako bila ruhusa, ukamtupia jiwe likampofua jicho, usingekuwa na kosa."

Kubisha hodi huzipa nyumba heshima yake, na huwalinda wakaazi wake na aibu na dhiki inayotokana na kushtukizwa, kuvamiwa ghafla, au kudhurika kwa kufichuka kwa siri. Na siri ni nyingi, si uchi wa mwili pekee kama wengi wanavyodhani. Bali hujumuisha pia siri za chakula, siri za mavazi, na siri za samani na mpangilio wa nyumba, ambavyo vina haki ya kuheshimiwa na kulindwa.

Mtu anayebisha hodi ni sunna kusalimia: "Assalamu alaykum, naweza kuingia?" Kupiga mlango kwa nguvu au kumpigia kelele mwenye nyumba ni haramu. Wanazuoni wa sharia ya Kiislamu wanasema, kuomba ruhusa kwa maneno yoyote yanayojulikana na jamii ni halali, alimradi hayako kinyume na sharia ya Kiislamu, lakini kufuata sunna ni bora zaidi.

Kadhalika, miongoni mwa adabu muhimu za kubisha hodi ni kuzingatia namna ya kusimama wakati wa kuomba kubisha hodi. Mgeni hapaswi kuelekeza uso wake mlangoni moja kwa moja, bali asimame upande wa kulia au kushoto wa mlango.

Adabu ya kubisha hodi inajumuisha pia jinsi ya kujitambulisha pale unapoulizwa: "Wewe ni nani?" Mgeni anapaswa kutaja jina lake, na si kusema tu: "Mimi." Hii inalingana na mfano wa malaika Jibril (amani imshukie) alipobisha hodi kwenye mlango wa mbingu usiku wa Mi'raj, alipoulizwa: "Nani?" Akajibu: "Jibril.

Watu wengi wa leo, licha ya kuwa ni Waislamu, hisia zao kuhusu adabu hizi nyeti zimepungua. Mtu anaweza kumvamia ndugu yake nyumbani kwake wakati wowote wa usiku au mchana, akagonga mlango mara nyingi bila kuchoka, na hatimaye hatoki mpaka awakere watu wa nyumba hiyo kiasi cha kulazimika kumfungulia.

Wakati mwingine mtu ana simu ambayo ingewezekana kabisa kupiga na kuomba ruhusa kupitia njia hiyo kabla ya kufika.

فتاوى رمضان

SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323

Mume kudai alipwe vitu alivyompa mke anayedai kujivua ndoa ni sawa?

Swali: **Mosi, Uislamu unamzungumziaje mume asiyetaka kumpa talaka mkewe kwa madai kuwa anajua kuoa tu hajui kuacha? Pili, mke akikataliwa kupewa talaka anaweza kuomba khului yaani kuvunja ndoa? Tatu, je hili suala la mume kukwamisha kutoa talaka mpaka arudishiwe misaada au vitu vyote alivyompa mkewe ni sawa?**

Jawabu: Swali lako ni zuri sana na la msingi linagusa misingi ya haki na maadili ya ndoa katika Uislamu, hasa pale mume anapogoma kumpa talaka mkewe na mke naye akachagua njia ya kujikhului (kujivua katika ndoa). Hebu tuchambue kwa mtiririko wa kifiqhi na kiushahidi ili jambo liwe wazi zaidi kwako:

Uislamu na talaka

Katika Uislamu, talaka ni haki ya mume, lakini ni haki yenye mipaka na masharti ya kimaadili. Allah anasema: "Talaka ni mara mbili; kisha ni kushikilia (ndoa) kwa wema au kuachana kwa ihsani." [Quran, 2: 229].

Aya hii inaweka misingi miwili muhimu: Kwanza, kama mume ataamua kubaki na mkewe, awe na nia ya kweli ya kumtendea wema. Msingi wa pili ni, kama ataamua kumuacha, basi afanye hivyo kwa ihsani, bila kudhulumu wala kumnyanyasa mkewe.

Kwa hivyo, mume haruhusiwi kutumia haki ya ndoa kama kifungo cha mateso au chombo cha kulipiza visasi. Allah anasema: "Wala msishikilie wake zenu kwa madhara, ili muwatese; kwani anayefanya hivyo amejidhulumu mwenyewe." [Qur'an, 2:231].

Kwa hivyo, mume anapomgomea mke kumpa talaka yake bila sababu ya kisheria, huku akimfanya aishi katika mateso, anakuwa anatumia vibaya haki aliyopewa na Sharia.

Kuhusu khului (mke kuomba kujivua kwenye ndoa)

Khului ni njia halali ya kuvunja ndoa ambapo mke huomba kuachwa na mumewe na kuwa tayari kurejesha mahari au sehemu yake. Mke anaruhusiwa kuomba kuvunja ndoa ikiwa hawezi tena kuendelea kuishi na mumewe kwa amani na kutimiza haki na wajibu wa kindoa.

Dalili ya haya tuliyoyabainisha ni kauli ya Allah Mtukufu: " T'alaka ni mara mbili. Kisha ni kukaa kwa wema au kuachana kwa vizuri. Wala si halali kwenu kuchukua chochote mlicho wapa wake zenu, ila ikiwa wote wawili wakiogopa ya kwamba hawataweza kushikamana na mipaka ya Mwenyezi Mungu. Basi mkiogopa kuwa hawataweza kushikamana na mipaka ya Mwenyezi Mungu hapo itakuwa hapana lawama ikiwa mwanamke atajikomboa. Hii ndiyo mipaka ya Mwenyezi Mungu; basi msiikiuke. Na watakaoikiuka mipaka ya Mwenyezi Mungu, hao ndio madhalimu." [Qur'an, 2:229].

Na pia imekuja kwenye hadith ya Ibn 'Abbas (Allah amridhie yeye na baba yake) kwamba mke wa Thabit bin Qays alikuja kwa Mtume wa Allah, (Allah amshushie rehema na amani) akasema: "Ewe Mtume wa Allah, simkatai mume wangu kwa dini wala tabia, lakini sipendi kuwa muasi baada ya kuwa ndani ya ndoa yake." Mtume wa Allah, akamuuliza: "Je, utamrudishia bustani aliyokupa kama mahari?" Akasema: "Ndiyo." Mtume (Allah amshushie rehema na amani) akamwambia Thabit: "Kubali bustani hiyo na muachie (mke wako)." [Bukhari].

Maana ya kauli hii ni kuwa kwanza, mke ana haki ya kuomba khului ikiwa hawezi kuvumilia tena maisha ya ndoa na pili, mume anapaswa kukubali, ikiwa anaona hakuna suluhisho la kindoa.

Kuhusu Mume kudai kila alichotoa

Hapa ndipo hoja yako kuu inapoingia. Allah anasema: "Talaka ni mara mbili. Kisha ni kukaa kwa wema au kuachana kwa wema. Wala si halali kwenu kuchukua chochote mlichowapa wake zenu ila wote wawili wakiogopa ya kwamba hawataweza kushikamana na mipaka ya Allah. Hapo itakuwa hapana lawama ikiwa mwanamke atajikomboa. Hii ndio mipaka ya Allah; basi msiikiuke. Na watakaoikiuka mipaka ya Allah, hao ndio madhalimu. [Qur'an, 2: 229].

Kisheria, mume hapewi haki ya kudai kurudishiwa kila msaada, zawadi, au matumizi aliyowahi kumpa mkewe. Anachostahiki kurudishiwa ni mahari tu au sehemu yake, au kusamehe kama masharti ya khului/ kuomba kuvunja ndoa yanavyoeleza.

Nao Ibn 'Umar na Ibn 'Abbas (Allah awaridhie wao na baba zao) walimsikia Mtume (Allah amshushie rehema na amani) akisema kuwa: "Haijuzu kwa mtu yeyote kutoa zawadi au hiba kisha akadai kurudishiwa, isipokuwa mzazi kwa kile alichompa mwanawe. Na mfano wa yule anayetoa zawadi kisha akadai kurudishiwa ni kama mfano wa mbwa aliyekula, kisha akishashiba hutapika, kisha hurudia tena matapishi yake." [Bukhari na Muslim].

TUJIFUNZE AI (ARTIFICIAL INTELLIGENCE)

Na Junaynat Ally Dama

'Prompt' ni msingi wa matokeo bora ukitumia AI

Katika zama hizi za akili mnemba (AI), watu wengi wanaanza kuitumia katika kuandika makala, kutafsiri, kufanya utafiti, kuandaa mipango ya biashara na hata kutengeneza mawazo mapya ya ubunifu.

Hata hivyo, kuna kanuni moja ya msingi ambayo watumiaji wengi huipuuzia: ubora wa matokeo ya AI hutegemea ubora wa maelekezo unayoiingiza. Kwa maneno mengine, "garbage in, garbage out" — ukiingiza taarifa au maelekezo mabovu, utapata matokeo mabovu.

'Prompt' ni nini?

Prompt ni maelekezo au swali unalolipa mfumo wa AI ili upate jibu. Ndiyo daraja linalounganisha akili yako na uwezo wa mashine. Kadiri maelekezo yanavyokuwa wazi, mahsusi na yenye mwelekeo, ndivyo AI inavyoweza kutoa majibu sahihi, yenye mpangilio na yanayokidhi lengo lako.

Watu wengi hufanya kosa la kuandika maneno machache yasiyoeleweka, kisha wanashangaa kwa nini majibu ni ya jumla au hayana kina. AI haisomi mawazo yako; inategemea kile ulichoandika.

Maelekezo mabaya majibu mabovu

"Garbage in, garbage out" ni kauli hii iliyoanzia katika sayansi ya kompyuta. Inamaanisha kuwa mfumo wowote wa kiteknolojia hauwezi kutoa matokeo mazuri kama data au maelekezo ya kuingiza ni mabovu. AI haibuni ukweli kutoka hewani; huchakata kile ulichowasilisha.

Kwa mfano, ukiandika: "Andika kuhusu biashara," utapata jibu la jumla sana. Lakini ukiandika: "Andika makala ya maneno 500 kuhusu changamoto za vijana kuanzisha biashara Tanzania, ukijumuisha takwimu na mapendekezo ya kitaalamu," utapata jibu lenye mwelekeo, hoja na mifano halisi.

Hapo ndipo nguvu ya maelekezo yako inaonekana.

Kwa nini prompt ni muhimu?

Kwanza, huongeza usahihi wa majibu. Maelekezo yaliyo wazi hupunguza uwezekano wa kupata taarifa zisizoendana na mahitaji yako. Pili, prompt huokoa muda. Badala ya kurekebisha majibu mara nyingi, unaanza na maelekezo sahihi tangu mwanzo.

Tatu, huongeza ubunifu. Ukieleza mtazamo unaoutaka—kwa mfano, mtazamo wa kitaalamu, wa kidini, au wa kijamii—AI inaweza kuunda maudhui yanayoendana na hadhira lengwa. Nne, huongeza udhibiti. Wewe ndiye unaongoza mwelekeo wa mazungumzo. AI ni chombo; prompt ndiyo usukani.

Sifa za prompt bora

Prompt bora ni ile ambayo inakidhi sifa nne. Sifa ya kwanza ni uwazi, ikimanisha epuka maneno ya jumla yasiyo na mwelekeo. Sifa ya pili ni umaalumu, yaani, maeleekezo yako yataje kwa urefu wa maandishi, hadhira, mtindo na madhumuni.

Sifa ya tatu ya prompt bora ni muktadha ikimaanisha utatakiwa utoe maelezo ya ziada yanayosaidia AI kuelewa lengo lako. Vilevile, zungumzia kuhusu muundo yaani eleza kama unahitaj vichwa vya habari, orodha au aya za kawaida.

Kadiri unavyoboresha ujuzi wa kuandika prompt (maelekezo), ndivyo unavyoboresha matokeo ya AI.

Msisitizo

Katika matumizi ya AI, watu wengi hudhani tatizo liko kwenye mfumo, ilhali mara nyingi tatizo liko kwenye maelekezo. Kanuni ya "garbage in, garbage out" inatukumbusha kuwa ubora wa matokeo hutegemea ubora wa kile tunachoingiza.

Upunjaji mizani: jinai inayohalalishwa kimyakimya katika jamii zetu

Tatfif katika maisha ya ndoa: mizani ya mapenzi, haki na uwajibikaji

Katika makala zilizopita, tumeona kuwa Tatfif (upunjaji mizani) huanzia sokoni, huingia kazini hususan katika taasisi na kisha hujipenyeza hadi ndani ya nafsi.

Lakini kuna eneo moja ambalo tatfif (upunjaji) hauonekani kirahisi, ilhali madhara yake huwa ya kina na ya kudum, eneo hilo ni ndani ya ndoa.

Ndoa hujengwa juu ya mizani nyeti: haki na wajibu, kutoa na kupokea, subira na kujitolea. Mizani hii inapopunjwa, hata kwa kiasi kidogo, huanza kutikisa misingi ya familia nzima.

Mara nyingi upunjaji huu hauanzi kwa migogoro mikubwa, bali kwa mabadiliko madogo ya tabia yanayorudiwa hadi kuwa mfumo.

Kudai haki kamili, kutekeleza wajibu nusu

Moja ya sura kuu za Tatfif (upunjaji) katika ndoa ni pale mmoja anapodai haki zote lakini anatekeleza wajibu kwa kiwango kidogo.

Mfano, mume anayetaka heshima, utiifu na utulivu, lakini hatimizi wajibu wa matunzo, ulinzi, ushauri mwema na upole. Mke naye anataka mapenzi, uaminifu na uwajibikaji, lakini hapendi kushiriki majukumu, kuheshimu mipaka ya ndoa au kulinda heshima ya familia.

Huu ni upunjaji wa wazi: unapima kwa kipimo kamili pale unapowakilisha madai lakini unapunguza unapotoa haki – kinyume na matakwa ya Uislamu ulioweka mizani ya haki kwa uwazi.

Katika Qur'an, Allah anatahadharisha vikali dhidi ya upunjaji mizani katika Suratul-Mutaffifin. Ingawa aya hizo zimetajwa katika muktadha wa biashara, mafunzo yake yanavuka soko na kuingia katika kila eneo la maisha ikiwemo ndoa.

Upunjaji wa hisia na muda

Upunjaji katika ndoa hauhusiani na mali pekee. Mara nyingi hutokea katika mambo yasiyopimika kwa macho ikiwemo kukosa muda wa mwenza, kunyima maneno ya faraja na mapenzi na kupuuzia mahitaji ya kihisia.

Mengine katika upunjaji wa kihisia ni kuendekeza simu kupita kiasi, kuzama kwenye tamthilia au kuchati kwenye mitandao ya kijamii, kuthamini zaidi kazi au marafiki mbele kuliko mwenza.

Hapa hakuna kelele, lakini mioyo hupata majeraha ya kudumu. Upunjaji (Tatfif) huua uhusiano, mawasiliano na heshima polepole bila wahusika kugundua mapema. Wakati mwingine mwenza hahitaji zawadi kubwa, bali uwepo wako; si pesa nyingi, bali maneno yenye uzito wa upendo.

Tatfif katika uongozi wa familia

Allah anasema katika Qur'an [4:34]: "Wanaume ni wasimamizi wa wanawake kwa sababu Allah amewafadhilisha baadhi yao juu ya wengine na kwa sababu ya wanayoyatoa katika mali zao..."

Aya hii haijatoa leseni ya ubabe, bali imeweka dhima ya uongozi kama amana. Uongozi wa familia si haki ya kujinufaisha, bali ni jukumu la kulinda mizani ya haki, rehema na uwajibikaji.

Tatfif hutokea pale uongozi unapotumiwa kama mamlaka badala ya jukumu. Mathalan, maamuzi hufanywa bila mashauriano, amri hutolewa bila mfano wa kuigwa, lawama hutolewa bila kujitathmini – alimradi mamlaka yanatumika kama silaha ya kimya au ya wazi.

Familia inayokosa mizani ya haki hugeuka uwanja wa migongano badala ya kuwa maskani ya sakina (utulivu wa nafsi).

Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) aliweka mfano wa uongozi wa huruma, akishauriana na wake zake na akisema: "Mbora wenu ni mbora kwa familia yake." Huu ndio mzani sahihi ya uongozi.

Athari za Tatfif katika ndoa

Tatfif (upunjaji) katika ndoa huzaa matokeo mazito ikiwemo kupotea kwa amani (sakina), kudhoofika kwa mawasiliano, kufa taratibu kwa mapenzi, watoto kulelewa katika mazingira ya mvutano na kuvunjika kwa ndoa kwa sababu zinazoonekana ndogo.

Mara nyingi talaka hazitokani na kosa moja kubwa, bali ni mkusanyiko wa Tatfif ndogo ndogo zilizopuuzwa kwa muda mrefu.

Watoto wanaokulia katika mazingira ya mizani iliyopunjwa hujifunza upunjaji huo kama mfumo wa kawaida wa maisha, na hivyo kuurithisha katika ndoa zao zijazo.

Kurejesha mizani ndani ya ndoa

Suluhisho la Tatfif (upunjaji) katika ndoa halipo kwenye madai, bali kwenye kujitathmini kwa dhati: Je, ninachodai ndicho ninachotoa? Je, namkumbuka Allah katika haki za mwenza wangu? Je, ninasamehe makosa madogo kama ninavyotaka nisamehewe? Je, ndoa yangu inaendeshwa kwa mizani ya haki au mizani ya maslahi binafsi?

Mizani hurudi pale kila mmoja anapoanza kupima nafsi yake kabla ya kumpima mwenza wake. Hatimaye ndoa inayorejesha mizani hupata baraka, hata kama changamoto hazikosekani.

Hakika, haki inapopewa nafasi yake, rehema hushuka, na pale rehema ilipo, sakina hurudi.

Hitimisho na muendelezo

Tatfif katika ndoa ni dhulma iliyojificha ndani ya kivuli cha upendo. Huonekana ndogo, lakini huacha majeraha makubwa. Na pale mizani inapopunjwa ndani ya familia, jamii nzima hulipa gharama.

Familia ndiyo kiini cha jamii. Ikiwa mizani itasimama sawa ndani ya nyumba, itasimama sawa pia katika soko, kazini na katika taasisi.

Katika makala inayofuata, tutachunguza Tatfif (upunjaji) katika elimu na malezi - kuanzia darasani hadi nyumbani - na namna upunjaji wa haki za elimu unavyoathiri kizazi cha sasa na kijacho.

Usikose makala inayofuata.

رمضان

MAKALA MAALUM

0712 690 811

NA SHEIKH SEIF RUGA

Makosa yafanywayo na baadhi ya wafungaji

Kujifunza sharia na hukumu za swaumu ni wajibu kwa Muislamu ili afunge kwa namna anayopenda na kuiridhia Allah Mtukufu, apate thawabu timilifu, na lengo la funga litimie, ambalo ni kumcha Allah Mtukufu.

Wapo wanaofunga swaumu ya Ramadhan lakini hawaufikii uchamungu kwa ujinga wao wa kutojifunza sharia, masharti na adabu za swaumu; vilevile kuna ambao inawalazimu kufungua kwa sababu ya maradhi hatari au udhuru wa kisharia, lakini wanaendelea kufunga na hivyo kuingia katika dhambi.

Kwa hiyo, kujifunza sharia za swaumu na hukumu zake ni wajibu wa lazima kwa kila aliyewajibishwa kufunga. Makala hii itaorodhesha baadhi ya makosa yanayofanywa na wafungaji wengi wa swaumu ya mwezi Mtukufu wa Ramadhan. Si nia yetu kutia dosari katika swaumu za watu au kuwakatisha tamaa, bali lengo ni kutanabahishana ili tujitahidi kuepuka makosa hayo. Na Allah ndiye mwenye kuwafikisha katika kheri.

Mosi: Kuupokea mwezi huu Mtukufu kwa vyakula vingi

Baadhi ya Waislamu huupokea mwezi Mtukufu wa Ramadhan kwa kununua vyakula na vinywaji vingi kupindukia, badala ya kujiandaa kwa utiifu.

Watu wenye tabia hii ya kufanya fujo ya matumizi wakumbuke kuwa wakati wakitumia kiasi kingi cha fedha kwa ajili ya kuyahudumia matumbo yao, kuna eneo si mbali na walipo wao kuna mafukara na masikini ambao hawapati hata tonge moja ya chakula itakayostawisha uzima wao.

Pili: Kuchelewa kufuturu na kuharakisha kula daku

Ni Sunna kuharakisha kufuturu mara tu inapothibitika kuingia wakati wa Magharibi, kwani Mtume wa Allah amesema: "Harakisheni kufuturu, na cheleweshеni kula daku."

Tatu: Kuacha kunuia usiku

Ni wajibu kutia nia ya kufunga swaumu ya Ramadhan wakati wa usiku. Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) amesema: "Asiyetia nia ya kufunga usiku, basi hana swaumu." Nia mahali pake ni moyoni, na kuitamka kwa ulimi ni kosa. Aidha, imekatazwa kwa aliyenuia kunywa au kula kwa makusudi wakati wa adhana ya Alfajiri ya kweli, na mwenye kufanya hivyo anakuwa ameharibu swaumu yake.

Nne: Kutozingatia au kutozijua fadhila za mwezi huu

Wapo baadhi yetu Waislamu ambao hawazijui fadhila za mwezi wa Ramadhan, kiasi cha kuupokea mwezi huu kama wanavyoipokea miezi mingine ya mwaka. Mtume wa Allah amesema: "Ramadhan ikiingia, hufunguliwa milango ya Pepo, hufungwa milango ya Moto, na mashetani (wakaidi) hutiwa pingu."

Tano: Kuacha kusali Sunna ya Tarawehe

Baadhi ya Waislamu hawaipi uzito Sunna ya Tarawehe katika usiku wa kwanza wa Ramadhan na hivyo kuacha kuisali. Hili ni kosa kubwa kwa sababu, mara tu unapoandama mwezi wa Ramadhan Muislamu anakuwa tayari ameingia katika usiku wa kwanza wa Ramadhan.

Sita: Baadhi ya wazazi kuwazuia mabinti zao kufunga

Wapo wazazi ambao huwazuia mabinti zao wenye umri mdogo kufunga wakidai kuwa ni wadogo. Kuhusiana na suala hili, Sheikh Ibn Jibrin (Allah amrehemu) amesema: "Wasichana wengi huanza kupata hedhi wakiwa na umri wa miaka 10 au 11, lakini wazazi wao huwapuuzia wakidhani bado ni wadogo."

Aidha, wapo baadhi ya wanawake ambao huacha kufunga wanapoona damu ya hedhi imekatika kabla ya Alfajiri na kabla ya kuoga wakidai kuwa alfajiri imewakuta bila kuoga. Hata hivyo, katika sharia ya Kiislamu, damu ya hedhi ikikatika wakati wa kuchomoza Alfajiri au kabla yake kidogo, mwanamke anawajibika kufunga na swaumu yake ni sahihi.

Saba: Wasiwasi mtu anapokula kwa kujisahau

Hutokea wakati mtu akapata wasiwasi anapokumbuka kuwa alikula au alikunywa kwa kusahau mchana wa Ramadhan, akidhani kuwa swaumu yake imeharibika. Mtume wa Allah amesema: "Anapokula au kunywa mmoja wenu kwa kusahau, basi akamilishe swaumu yake, kwani Allah Mtukufu ndiye aliyemlisha na kumnywesha."

Nane: Kupaka hina, wanja, dawa ya matone

Swaumu ya mtu haibatiliki kwa kupaka chochote miongoni mwa vitu hivi. Haibatiliki funga kwa kupaka hina, dawa ya matone ya sikio au hata macho.

Tisa: Kuhofia kuonja chakula jikoni

Wanawake wengi huhofia kuonja chakula jikoni kwa kuogopa kuharibu swaumu zao. Katika kulielezea hili, Sheikh Ibn Jibrin (Allah amrehemu) amesema: "Hakuna ubaya kuonja chakula kwa haja, kwa kukiweka kwenye ncha ya ulimi ili kujua ladha yake, bila kumeza chochote. Swaumu yake (mtu huyo) haiharibiki."

Kumi: Kutofahamu sharia za swaumu na hukumu zake

Muislamu anatakiwa ajue namna ya kutekeleza ibada kabla ya kuingia kwenye ibada husika. Hivyo katika mwezi wa Ramadhan, Muislamu anatakiwa ajifundishe Hukumu, Sharti, Nguzo, Adabu, Wajibu, Sunna na mambo mengine yahusuyo swaumu ili atekeleze ibada hii adhimu kikamilifu na kwa ufanisi.

Kumi na moja: Kupiga mswaki mchana wa Ramadhan

Waislamu wengi huacha kupiga mswaki mchana wa Ramadhan kwa hofu ya kuharibu swaumu zao. Juu ya hilo, Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) amesema: "Lau kama si kuhofia kuupa uzito umma wangu, ningewaamuru wapige mswaki kabla ya kila swala." [Bukhari, Muslim, Abu Daudi, na wengineo].

رمضان

MUSSA IMANI SHEHA ZANZIBAR
0773 181 494

SEHEMU YA 1

VISA VYA MITUME NA MASWAHABA

SIMULIZI YA AKINA THAMOUD WATU WA NABII SWALEH

Akina Thamoud waliwarithi kina Adi kama ambavyo kina Adi walivyowarithi watu wa Nabii Nuhu. Inasemekana kabila la akina Thamoud liliishi eneo lililojulikana kwa jina la Hijr lililopo kati ya Madina na Tabouk ambako kwa sasa panaitwa "Mada'in Swaleh."

Akina Thamoud walibarikiwa ardhi nzuri ya kilimo yenye rutba, iliyojaa mito na chemchem. Wakaimarisha ardhi hiyo kwa mashamba na mabustani mazuri, hadi neema zikawaenea kila upande.

Thamoud waliwapita akina Adi kwa akili na ufundi (teknolojia), wakaweza kuitoboa milima mirefu na kutengeneza humo majumba makubwa ya fahari, ambayo katika kuta zake walichora nakshi za kuvutia.

Yoyote aliyeingia ndani ya mji wao alishuhudia maajabu makubwa ya kiufundi: makasri marefu, mabustani yaliyopambwa na miti mirefu ya matunda na vivuli vikubwa, majina yavutiayo na maua mazuri.

Kiujumla, Mwenyezi Mungu aliwafungulia Thamoud baraka za mbinguni na ardhini, na kila mlango wa neema. Qur'an, katika sura mbalimbali, imesimulia habari za kina Thamoud, ambazo zina mazingatio makubwa kwa wanaotaka kuonyeka.

Kwa mfano katika Qur'an [89:9] inasema: "Na Thamoud waliochonga majabali (wakayafanya majumba) katika uwanja wao."

Kufuru ya akina Thamoud

Maisha ya baraka na neema hayakuwapelekea Thamoud kumtambua, kumshukuru na kumuabudu Mola wao. Walizifurahia tu neema hizo, huku wakijiingiza katika dhambi na kumsahau mneemeshaji.

Kiburi kiliwapanda vichwani mwao, kama kilivyowapanda watu wa Mtume Hud (amani ya Allah imshukie), nafsi zao zikawahadaa wakadhani kuwa neema walizonazo ni milki yao, ni za milele na wala hazitakwisha.

Si hivyo tu, walidhani kwamba, kifo hakiwezi kuingia katika majumba yao ya mawe. Walijiaminisha kuwa hakuna balaa ama nguvu yoyote inayoweza kuwashinda.

Ibada zao

Kama walivyokuwa watu wa Mtume Nuhu na kina Adi, ilikuwa hivyo hivyo kwa wakina Thamoud ambao na waliabudu masanamu waliyoyatengeneza kwa mikono yao kutokana na mawe.

Angalia ujinga na upotofu wa mwanadamu anapokosa Tauhid!!! Allah aliwalainishia majabali wakayatawala na wakayasarifu na kuyasanifu wapendavyo, lakini kwa ujinga wao wakayaabudu, wakajidhalilisha na kujinyenyekesha mbele yake!

Hivi mwenye nguvu anamuabudu dhaifu!? Bwana anamsujudia mtumwa?! Mwenye akili timamu anajitiisha mbele ya kisicho na akili!?

Swaleh alingania watu wake

Akina Thamoud wakiwa wametopea katika ushirikina, starehe, upotofu pamoja na anasa zao, Allah akataka kuwaongoza na kuwatoa katika giza la ujinga, dhulma na kujisahau na kuwaleta katika nuru ya Tauhid, elimu na kujielewa.

Katika mji wao alikuwepo mtu mwenzao aliyeitwa Swaleh, mzawa na mzalendo. Tokea utotoni mwake, Swaleh alikuwa mtu mwema (kama jina lilivyoakisi), mwerevu, mwenye akili kubwa na mtazamo wa mbali.

Watu walimjua na sifa zake, wakamjengea matumaini makubwa kuwa atakuwa ndio sharif (mtukufu/kiongozi) wao, na mtatuzi wa changamoto zao. Kadhalika, waliyatazama maisha yake ya baadae kwamba yatakuwa ya kifahari kupita wao, na angekuwa kiongozi wa ibada zao potofu za kusujudia sanamu.

Kutokana na muktadha huo, Swaleh alipowajia na kuwataka wamuamini na wamuabudu Allah peke yake, walimshangaa na kumuona kama mtu aliharibikia ukubwani.

Tuirejee Qur'an: "Wakasema: ewe Swaleh, kwa kweli ulikuwa mtu wa kutumainiwa kati yetu (lakini sasa ushaharibika), yaani unatukataza kuabudu waungu waliowaabudu wazee wetu!? Na sisi tuna mashaka na wasiwasi (na ukweli wa) hayo unayotuitia." [Qur'an, 12:62].

Pahala pengine, Qur'an inasema: "Na kwa Thamoud tulimpeleka ndugu yao Swaleh, akasema, 'Enyi watu wangu, muabuduni Mwenyezi Mungu. Nyinyi hamna mola ila Yeye... Na kumbukeni Allah alivyokufanyeni makhalifa baada ya Adi na kukuwekeni vizuri katika ardhi, mnajenga majumba makubwa ya kifalme katika nyanda zake, na mnachonga majumba katika majabali. Basi, zikumbuke (zizingatieni) neema za Mwenyezi Mungu wala msifisidi katika ardhi na kufanya uharibifu.'" [Qur'an, 7: 73-74].

Na pahala pengine, Qur'an inasimulia: "Na kwa Thamoud tukampeleka Swaleh, akasema, 'Enyi watu wangu, muabuduni Mwenyezi Mungu. Nyinyi hamna mungu ila Yeye. Yeye ndiye aliyekuumbeni katika ardhi na akakukalisheni humo, basi muombeni msamaha kisha rejeeni Kwake. Hakika Mola wangu yu karibu (na waja wake) anapokea (maombi)." [Qur'an, 12:61].

Toleo linalofuata tutaona majibu ya kina Thamoud inshaAllah.

رمضان

NASAHA ZA WIKI 0787 503 085

NA YUSUFU AMINI

Ramadhan, msimu adimu wenye fursa ya kipekee

Tumeanza kutekeleza ibada ya swaumu ya Ramadhan, ambayo ni nguzo ya nne katika Uislamu. Tunafahamu kuwa mfanyabiashara anapoingia sokoni anataraji kupata faida kutokana na mauzo ya bidhaa au huduma anayotoa. Vivyo hivyo katika soko la Ramadhan, wafanyabiashara hupata fursa ya kuuza bidhaa zao kwa haraka na kwa bei ya juu.

Katika soko hili, mteja ni mmoja tu: Mwenyezi Mungu Mtukufu, ambaye hununua bidhaa na kuzihifadhi kisha anaziongezea ubora na faida. Faida kubwa zaidi ya soko la Ramadhan itaonekana Siku ya Kiyama pindi Mwenyezi Mungu atakapowarudishia wenyewe bidhaa zao ambapo watakuwa wanazihitaji sana.

Mwenyezi Mungu anasema: "Na chochote cha kheri mnachokitanguliza kwa ajili ya nafsi zenu mtakikuta mbele ya Mwenyezi Mungu kikiwa bora na ujira mkubwa zaidi..." [Qur'an, 73:20].

Tunapofanya biashara na Allah, tunatakiwa tuepuke kutumia aina yoyote ya ghushi (ubabaishaji). Nasema hivyo kwa sababu, kwanza, Allah hapendi bidhaa isiyo na kiwango. Pili, anatujua vyema kuliko tunavyojijua wenyewe, na hatuna namna yoyote ya kumdanganya.

Katika hadith iliyonukuliwa na Muslim, Mtume (rehema za Allah na amani imshukie) amesema: "Hakika Mwenyezi Mungu ni Mzuri na hakubali ila kilicho kizuri." Pia Mtume amesema: "Mwenyezi Mungu anapenda mmoja wenu akifanya amali yoyote aifanye vizuri." [Abu Ya'laa].

Kwa kuwa soko la Ramadhan ni la muda mfupi (siku 29 au 30), inatarajiwa kila mfanyabiashara (Muislamu) atakusanya bidhaa kwa ajili ya mteja wake (Allah Aliyetukuka) ambaye ni tajiri mno. Natumai sote tutachangamkia fursa hii na kushindana kuuza bidhaa nyingi usiku na mchana.

Watakaofaidika na soko la Ramadhan ni wale walioshtushwa na taarifa ya kufunguliwa kwa soko na kulitumia vema. Bidhaa watakazouza Waislamu hawa ni pamoja na sala za jamaa, Qiyam Ramadhan, zaka/ sadaka, na usomaji Qur'an. Bidhaa nyingine ni pamoja na dhikri na dua, kufuturisha, kufariji wasiojiweza, kuamrisha mema na kukataza mabaya.

Watakaopata hasara

Kama tujuavyo, katika mwezi wa Ramadhan malipo huzidishwa na makosa hufutwa kwa wale wenye kumuomba Allah msamaha na kutubia kwake. Kwa hiyo, Muislamu atakayeudiriki mwezi wa Ramadhan kisha akawa hajasamehewa madhambi yake, huyo atapata hasara kubwa.

Kwa kulijua hilo, Mtume (rehema za Allah na amani imshukie) alikuwa akiwaambia Masahaba wake kila unapoingia mwezi wa Ramadhan: "Hakika umekujieni mwezi

wa Ramadhan, mwezi uliobarikiwa. Allah amefaradhisha juu yenu kuufunga, hufunguliwa ndani yake milango ya Pepo na hufungwa ndani yake milango ya Moto, na mashetani (wakaidi) hufungwa minyororo, ndani yake (mwezi huo) kuna usiku ambao ni bora kuliko miezi elfu moja. Atakayenyimwa kheri zake (usiku huo), hakika huyo amenyimwa kheri zote." [Ahmad].

Tunafahamu kuwa kila biashara ina sababu zake za kupata faida. Miongoni mwa sababu hizo ni kuandaa mahala pazuri pa kufanyia biashara, kuwa na bidhaa nzuri na zenye thamani, kuhakikisha bidhaa haiharibiki, kuifanya iwe na mvuto kwa wateja, pamoja na kuwa na muamala mzuri na wateja.

Haya yote tunayatenda na kuyahangaikia pale tunapohitaji faida za kilimwengu. Kwa kuwa Ramadhan ni msimu wa kufanya biashara na Allah Ta'ala, tunatakiwa tujitahidi kutenda mambo mema na kuyapa thamani kwa kufuata utaratibu unaotakiwa, kwani Allah haridhii ila yaliyokuwa mazuri na hakubali isipokuwa yale yaliyofanywa kwa utakasifu wa nia.

Ramadhan ni msimu wa kutenda, hivyo tujitahidi kutenda mambo mema na yenye ubora mbele ya Allah ili tupate msamaha na radhi zake. Pia tushindane kufanya heri ili tujikurubishe kwa Allah Ta'ala. Allah anasema: "Na wa mbele watakuwa mbele. Hao ndiyo watakaokaribishwa. Katika bustani zenye neema." [Qur'an, 56:10–12].

Kwa kuwa soko la Ramadhan ni la muda mfupi, tunapaswa kutangaza na kuuza bidhaa zetu kwa Allah Ta'ala kwa bei nzuri. Yeyote atakayeacha kuuza bidhaa zake kwa Allah, hakika huyo atapata hasara kubwa. Madhila yaliyoje kwa anayezembea kufanya ibada ndani ya Ramadhan.

Hadith aliyoisimulia Abi Huraira (Allah amridhie) inaeleza kuwa, siku moja Mtume (rehema za Allah na amani iwe juu yake) alipanda katika mimbari akasema: "Aamin..., "Aamin..., "Aamin." Akaambiwa: "Ewe mjumbe wa Allah, hukuwa unafanya hivi." (Mtume) akasema: "Jibril ameniambia, 'Amepata hasara mtu ambaye Ramadhan imemkuta (kisha ikamalizika) asisamehewe,' nikasema, 'Aamin.'

Kisha (Jibril) akasema, 'Amepata hasara mtu ambaye umetajwa mbele yake asikuswalie (kukutakia rehema na amani),' nikasema, 'Aamin.' Kisha akasema, 'Amepata hasara mtu aliyewadiriki wazazi wake wawili au mmoja kati yao halafu asiingie Peponi', nikasema, 'Aamin.'" [Imenukuliwa na Bukhari, Bayhaqi na Ahmad].

Hakika, kuna watu wengi wanaotoka ndani ya Ramadhan wakiwa wamefilisika. Hawa ndio aliowazungumzia Mtume kuwa, hawana fungu wanalolipata zaidi ya kushinda na njaa na kiu. Maisha yao yatakuwa vilevile kama walivyokuwa kabla ya Ramadhan.

Tusipokuwa na maisha yanayofanana na kile tunachojifunza ndani ya funga, itakuwa ni kielelezo tosha kuwa ibada zetu zina kasoro kubwa inayosababisha kutokuwa na taathira yoyote katika maisha yetu.

Ukweli mchungu ni kwamba, wengi wetu, ama kutokana na uvivu, uzembe au kupuuza ibada za Sunna, tumekuwa hatujishughulishi na ibada za usiku (Qiyam Llayl), kusoma Qur'an, kusaidia wenye shida na kadhalika. Tunasahau kuwa uhusiano wetu na Mwenyezi Mungu upo katika kufuata Sunna za Mtume wake (rehema za Allah na amani imshukie).

Katika hadithil Qudsy, Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: "...Mwanadamu hutaweza kuyafikia yaliyoko kwangu ila kwa kutekeleza yale niliyokufaradhishia juu yako, wala hatajikurubisha kwangu kwa Sunna ila nitampenda..." [Bukhari].

رمضان

MAKALA MAALUM
0773 181 494

MUSSA IMANI SHEHA, ZANZIBAR

Ujumbe kwa Wasomi Waislam

Uislamu ni dini ya elimu, na imepiga vita ujinga tokea mwanzo wa risala (ujumbe) yake kwa walimwengu. Aidha, Uislamu umehimiza kusoma elimu zote zenye manufaa kwa mwanadamu.

Uislamu hautenganishi elimudini na elimudunia. Kila elimu ina nafasi yake katika maisha ya mwanadamu alimradi iwe kwa ajili ya Muumba. Na mtaalamu wa fani yoyote ni hitajio la jamii inayomzunguka kwa ustawi wake.

Lakini kuna elimu ya msingi na ambayo kila Muislamu anapaswa kuijua, nayo ni elimu ya dini, ambayo ndio muhimili na msingi wa elimu zote.

Hii ni elimu ya kumtambua Allah Muumba na ulazima wa kumtumikia. Elimu ya kumjuvya mwanadamu haki na majukumu yake kwa viumbe wenzake kiimani, na kumuongoza kuwa na tabia njema, na kujali shida za wengine.

Hali ya jamii

Jamii leo inaonekana kuvutika sana na elimu ya mazingira ama "elimuajira." Juhudi wanazozifanya wazazi za kuhakikisha watoto wao wanaipata elimu ya mazingira hatimae kupata ajira ni kubwa sana, na huanza mapema kabisa. Hupitia ngazi zote: maandalizi, msingi, sekondari hadi chuo.

Lakini kwa upande wa masomo ya dini, juhudi hizi hazionekani sana - si kwa wazazi wala kwa hao watoto na vijana wenyewe waliokwisha kuisoma picha na kujua nini haswa wanachokihitajia wazazi wao.

Matokeo yake

Matokeo ya upuuzaji huu mkubwa wa elimu ya kiroho ni kuwa na idadi kubwa ya wasomi Waislamu, bobezi katika fani mbali mbali katika elimu ya mazingira lakini wana uelewa mdogo sana kuhusu dini yao.

Aghlab, mambo huharibika na haki za watu kupotea pale wasomi hao wanapopewa dhamana ya kuwa viongozi na watumishi wa umma kama wanasiasa, madaktari, walimu, viongozi wa umma, askari, walinzi, wanahabari, mahakimu, wanasheria, mawakili nk.

Utashi na tamaa za kujipatia maslahi, huushinda utu, huruma na kujali shida za watu. Uzembe, utapeli, rushwa, majungu na hata ushirikina kazini, uongo, na hiyana: huwatawala wasomi hao.

Pia, hawasalimiki na wizi wa mali ya umma pale wanapoamini kuwa hakuna jicho la mtu au chombo cha sheria kinachowamulika . Jamii yenye wasomi na watendaji kama hao hujikuta inanyonywa na kubeba mzigo mzito usio na faida kwake, na maisha ya wanajamii kuwa magumu zaidi.

Upuuzaji wa maagizo ya Allah –kama vile swala- kwa wasomi hao ni kitu cha kawaida. Baadhi yao hufikia hatua ya kuwadharau waliosoma dini, wakajawa na kibri na kutoa lugha za kejeli dhidi ya Uislamu (dini yao wenyewe) na viongozi wake.

Wasomi hao hujiliwaza: eti kwa vile wamesoma sana fani zao mbali mbali, basi hata dini nayo wanaijua, na wana uwezo wa kuisemea wakitaka wakitegemea mantiki badala ya Qur'an na Sunna kwa ufahamu wa wema waliotangulia.

Kuathirika na umagharibi

Mtihani zaidi ni wasomi hao kuathiriwa na nadharia za wasio Waislamu (hasa ulimwengu wa kimagharibi) wakawapenda na kuwasifia kuliko Waislamu wenzao.

Huzimeza historia, tafiti na nukuu za watafiti na vumbuzi zao, lakini wanashindwa kujua historia ya Mtume (Allah amshushie rehema na amani) na Maswahaba wake (Allah awaridhie), wala hawawezi kunukuu aya, hadith au kauli za wataalamu (wasomi) wa Kiislamu.

Tazama ndugu zetu hawa –Allah atuongoze sisi na wao-wanavyokuwa wageni siku zote katika utekelezaji wa ibada misikitini. Naam, kwa sababu hawajifunzi na wala hawana mpango wa kujifunza!

Pitia darsa za misikitini, mihadhara ya dini pamoja na taasisi za maarifa ya Uislamu, halafu angalia washiriki wa programu hizo ni akina nani? Hatutarajii kwamba, utawaona wengi katika waitwao wasomi na ambao wana ajira (nyadhifa) zao kubwa kubwa au wenye vipato vikubwa (matajiri).

Haitarajiwi pale kuwakuta: wakurugenzi, makatibu wakuu, wabunge, mawaziri, maafisa, mameneja, wakuu wa mikoa na wilaya nk. ambao ni waislamu, ambao walipaswa pia kujifunza na kuijua vyema dini yao!!

Wito

Tunatoa wito kwa wazazi kuwapeleka watoto wao katika taasisi za elimu ya dini (madrasa na ma'had) wakajifunze imani iwasaidie katika kujenga mahusiano mema na Mola wao, na kuwa raia wema wasiwe mzigo kwa wanajamii wenzao.

Tunawaambia ndugu zetu waliosoma elimu ya mazingira (sekula) na kushika nyadhifa mbali mbali, na ambao hawakubahatika kuijua dini yao: bado hawajachelewa.

Muda bado upo na wajibu uko pale pale. Wajishuhulishe na kuisoma dini yao kwa namna majukumu yatakavyowaruhusu. Kuweni karibu na wasomi wa dini mubadilishane uelewa kwani elimu ni bahari.

Saidianeni katika kuwaongoza watu njia iliyo sahihi. Jamii inawategemea sana, ioneeni huruma. "Mbora wa watu ni awatumikiae watu."

JUNAYNAT ALLY DAMA

WHO: Kesi nne kati ya kumi za saratani duniani zinaweza kuzuilika

Kila tarehe 4 Februari, dunia huadhimisha Siku ya Saratani Duniani. Siku hii inalenga kuongeza uelewa kuhusu ugonjwa wa saratani na kusisitiza umuhimu wa kinga, uchunguzi wa mapema na matibabu.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka kurasa rasmi za Shirika la Afya Duniani (WHO), kuna habari njema yenye kutia moyo: hadi kesi nne kati ya kumi za saratani duniani zinaweza kuzuilika.

Uchambuzi wa kimataifa uliofanywa na WHO kwa kushirikiana na Wakala wa Kimataifa wa Utafiti wa Saratani (IARC) unaonesha kuwa mwaka 2022 pekee, takribani kesi milioni 7.1 za saratani zilihusishwa na sababu zinazoweza kuzuilika. Hii ina maana kwamba mamilioni ya watu wangeweza kuepuka ugonjwa huu kwa kufanya mabadiliko ya mtindo wa maisha na kupitia hatua madhubuti za afya ya umma.

Miongoni mwa vihatarishi vikubwa vinavyochangia saratani, matumizi ya tumbaku yanaongoza. Tumbaku inahusika na asilimia 15 ya visa vipya vya saratani duniani. Uvutaji sigara na matumizi mengine ya tumbaku huongeza hatari ya saratani ya mapafu, koo, mdomo na viungo vingine. Kuacha kuvuta sigara au kutokuanza kabisa ni hatua muhimu inayoweza kuokoa maisha. Maambukizi pia ni chanzo kikubwa cha saratani. Virusi kama HPV (Human Papillomavirus) na homa ya ini aina ya B na C vinachangia takribani asilimia 10 ya visa vipya vya saratani.

HPV inahusishwa sana na saratani ya mlango wa kizazi kwa wanawake, huku maambukizi ya homa ya ini yakichangia saratani ya ini. Chanjo dhidi ya HPV na homa ya ini B ni njia salama na yenye ufanisi ya kupunguza hatari hizi.

Matumizi ya pombe yanachangia takribani asilimia tatu ya visa vipya vya saratani. Ingawa baadhi ya watu huchukulia pombe kama sehemu ya burudani ya kawaida, matumizi yake kupita kiasi huongeza hatari ya saratani ya ini, matiti, koo na sehemu nyingine za mwili. Kupunguza au kuacha kabisa matumizi ya pombe ni hatua nyingine muhimu ya kinga.

Sababu nyingine zinazoweza kuzuilika ni pamoja na uchafuzi wa hewa, kutofanya mazoezi ya mwili, uzito kupita kiasi na kukaa muda mrefu juani bila kinga. Uchafuzi wa hewa huathiri hasa afya ya mapafu.

Kutofanya mazoezi na kuwa na uzito mkubwa huongeza hatari ya saratani mbalimbali, ikiwemo ya utumbo mpana na matiti. Aidha, mionzi ya jua (UV) huongeza hatari ya saratani ya ngozi, hasa kwa watu wanaokaa juani bila kujikinga.

Kwa mujibu wa takwimu hizo, saratani ya mapafu, tumbo na mlango wa kizazi zinachangia karibu nusu ya visa vyote vya saratani vinavyoweza kuzuilika. Hii inaonyesha kuwa kwa kuchukua hatua sahihi, tunaweza kupunguza kwa kiasi kikubwa mzigo wa ugonjwa huu katika jamii zetu.

Je, mtu mmoja anaweza kufanya nini? Kwanza, epuka matumizi ya tumbaku na punguza au acha kabisa pombe. Pili, fanya mazoezi mara kwa mara na hakikisha unadumisha uzito unaofaa. Tatu, pata chanjo dhidi ya HPV na homa ya ini B kulingana na ushauri wa wataalamu wa afya. Nne, linda ngozi yako dhidi ya mionzi ya jua kwa kuvaa mavazi yanayofunika mwili na kutumia kinga ya jua.

Saratani si hukumu isiyobadilika. Ingawa si visa vyote vinaweza kuzuilika, sehemu kubwa ya hatari inaweza kupunguzwa kupitia maamuzi sahihi ya kila siku na sera madhubuti za afya ya umma.

Siku ya Saratani Duniani ni ukumbusho kwamba kinga ni silaha yenye nguvu. Tukishirikiana kama jamii—serikali, taasisi za afya na wananchi—tunaweza kupunguza hatari ya saratani na kujenga kizazi chenye afya bora.

MATUKIO YENYE MAZINGATIO

NA ZAHARANI BARAKA

Siri za kula kiafya katika Ramadhan

Imepokewa hadith kutoka kwa Abu Huraira (Allah amridhie) kwamba, kulikuwa na mtu mmoja anayekula chakula kingi mno, baadaye akaingia katika Uislamu, akawa anakula chakula kichache. Jambo hilo likatajwa mbele ya Mtume (Allah amshushie rehema na amani), naye akasema: "Hakika muumini anakula katika utumbo mmoja, na kafiri anakula katika matumbo saba." [Sahih Bukhari].

Hadith nyingine iliyonukuliwa na Bukhari kutoka kwa Nafi'i, mtumwa wa Abdullah bin Umar (Allah amridhie) inaeleza kuwa, Ibn Umar (Allah amridhie) alikuwa na mazoea ya kutokula mpaka masikini aletwe kwake wale pamoja. Siku moja Nafi'i alimleta mtu ale pamoja na Ibn Umar, lakini mtu huyo akala sana.

Ibn Umar akasema: "Ewe Nafi'i, usimwingize tena mtu huyu kwangu. Nilimsikia Mtume (Allah amshushie rehema na amani) akisema: 'Muumini anakula katika utumbo mmoja, na kafiri anakula katika matumbo saba.'"

Mafundisho ya tukio

Unapoingia mwezi Mtukufu wa Ramadhan mambo mengi hubadilika ikiwa ni pamoja na ulaji usiofaa. Muislamu anatakiwa kujizuia kula na kunywa mchana kutwa wa mwezi wa Ramadhan, na awe mvumilivu kwa ajili ya kutaka radhi za Allah kwa kuchunga na kuzingatia miiko ya funga mpaka jua linapozama wakati wa Magharibi.

Lakini, shukrani ya dhati kabisa kwa Muislamu anayefunga swaumu ya Ramadhan ni kuwa na matumizi sahihi ya neema ya vyakula na vinywaji kwa kufuata muongozo na taratibu za kisheria.

Hakuna kinachobadilika katika kula, utaratibu ni ule ule

Funga ya Ramadhan haibadilishi mfumo wa ulaji, bali inabadilisha muda na nyakati ambazo Muislamu ameruhusiwa kula na nyakati ambazo haruhusiwi. Maisha ya Muislamu ndani ya Ramadhan yanapaswa kufuata mfumo ule ule wa maisha yake ya kila siku katika upande wa kula na kunywa.

Muislamu anatakiwa afuturu na kula daku kwa kuzingatia adabu za kula ambazo zimefafanuliwa kwa kina katika mafundisho ya Uislamu, lakini pia ajiepushe na mambo yote ambayo hapaswi kuyafanya wakati wa kula futari na daku.

Kutokana na kukaa kipindi kirefu bila kula chochote katika mchana wa Ramadhan, baadhi ya watu hukiuka taratibu za Uislamu wakati wa kufuturu na kula daku.

Ni kwa sababu hiyo, Mtume (Allah amshushie rehema na amani) ametoa muongozo na maelekezo kwa waumini kuhusiana na suala la kufuturu na kula daku kwa maslahi ya afya zao, na ili waone kuwa hiyo ni sehemu ya ibada kwao. Ikiwa tumepewa muongozo wa kula vitu vizuri kwa afya ya mwanadamu, tutambue kuwa hata ulaji mbaya nao umekatazwa kisheria.

Muumini anakula katika utumbo mmoja: Huu ni mfano unaomaanisha kuwa muumini anakula kwa adabu, kwa kiasi, bila tamaa wala pupa. Anaridhika na kidogo, na Allah Ta'ala hukibariki chakula chake.

Kafiri anakula katika matumbo saba: Hii ni taswira ya mtu anayekula kwa tamaa, pupa, uchu na kufuata matamanio yake bila kujali mipaka. Kafiri hula sana na hivyo kukosa baraka na rehema za Allah. Hiyo haina maana kwamba muumini ana utumbo mmoja na kafiri ana matumbo saba, bali ni mfano wa muumini kuridhika na kiasi, na kafiri kuwa na tamaa.

Kula kiasi ni muhimu kwa afya

Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Mwanadamu hajapata kujaza chombo kibaya kuliko tumbo. Yamtosha mwanadamu vitonge (vya chakula) vya kunyoosha uti wake wa mgongo (kumpa uhai). Na ikiwa ni lazima kufanya hivyo; basi theluthi moja ni ya chakula chake, theluthi moja ya kinywaji chake, na theluthi moja ya pumzi yake." [Ahmad na Tirmidhi].

Hadith inaonesha umuhimu wa kula kwa mpangilio na kiasi (kipimo), si kula kila kitu kwa sababu tu kinapatikana, au una uwezo wa kukinunua. Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Chakula cha mtu mmoja kinawatosha watu wawili, na cha wawili kinawatosha wanne, na cha wanne kinawatosha wanane." [Muslim].

Ajabu ni pale mtu mmoja anapokula chakula cha watu wawili au watatu kiasi cha kumfanya ashindwe hata kujibidiisha katika ibada zinazopatikana ndani ya mwezi wa Ramadhan.

Kufuturisha pasina kufanya israfu

Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) alikuwa mkarimu mno, kama ilivyothibiti katika hadith ya Ibn Abbas (Allah amridhie) ambaye amesema: "Mtume (Allah amshushie rehema na amani) alikuwa mkarimu mno kwa watu, na ukarimu wake uliongezeka zaidi ndani ya Ramadhan alipokutana na Jibril, na alikuwa akikutana nae kila usiku wa Ramadhan. Kwa hakika mjumbe wa Allah alikuwa akijitolea katika kheri kuliko upepo uliotumwa." [Bukhari].

Na miongoni mwa sadaka zinazotiliwa mkazo katika mwezi wa Ramadhan ni kumfuturisha aliyefunga. Mtume amesema: "Atakayemfuturisha aliyefunga anapata malipo (thawabu) mfano wa malipo ya aliyemfuturisha, na hakipungui chochote katika malipo ya mfungaji." [Tirmidhi]. Kwa hiyo, usichoke kuwaandalia futari nzuri wanafamilia na wale wote unaomudu kuwasaidia.

Israfu kwenye meza ya chakula

Kufanya israfu, maana yake ni kuleta fujo kwa aina yoyote ile – ima kula chakula kingi zaidi ya hitajio la mwili, au kufanya matumizi ya ziada yasiyokuwa na sababu, au kupika vyakula vingi ambavyo hatimaye husazwa na kuishia kwenye madebe ya taka.

Allah 'Azza Wajallah' anasema: "Na Yeye ndiye aliyeziumba bustani zenye kutambaa juu ya chanja, na zisizotambaa, na mitende, na mimea yenye matunda mbalimbali, na mizaituni na mikomamanga inayofanana na isiyofanana. Kuleni matunda yake inapozaa, na toeni haki yake siku ya kuvunwa kwake. Wala msitumie kwa fujo. Hakika Yeye (Allah) hawapendi watumiao kwa fujo." [Qur'an, 6:141].

Allah akasema tena: "Enyi wanadamu! Chukueni pambo lenu katika kila pahala wakati wa ibada, na kuleni, na kunyweni na wala msifanye ubadhirifu. Kwa hakika Yeye (Allah) hawapendi wafanyao israfu." [Qur'an, 7:31].

IDARA YA DAAWA

Mtume ﷺ

amesema:

"Muislamu ni yule ambaye Waislamu wengine wamesalimika kutokana na ulimi wake na mkono wake, na Muhajir (mhamaji wa kweli) ni yule anayeacha kile alichokataza Mwenyezi Mungu."

Bukhari

www.islamicftz.org

JUNAYNAT ALLY DAMA

Tuwaongoze watoto katika matumizi bora vifaa vya mawasiliano kidijitali

Katika Dunia ya leo, teknolojia ya mawasiliano ya kidijitali imekuwa sehemu ya maisha. Wakati baadhi yetu wa umri mkubwa ni wahamiaji, kwa watoto ni mazingira ya kawaida kwani wamezaliwa katikati ya mapinduzi haya.

Madhara ya teknolojia hizi za mawasiliano yameelezwa sana kuanzia uraibu, uharibifu wa maadili, hadi madhara kwa afya ya macho, akili na kadhalika. Swali ni je tunawakingaje watoto na madhara haya? Jibu rahisi ni kuwazuia kabisa kutumia vifaa hivi.

Hata hivyo, ni busara kufanya kuzuia watoto wasitumie kabisa vifaa vya kieletroniki vya mawasiliano na je inawezekana? Licha ya hasara lukuki, kuna faida lukuki na nyingi zinazopatikana kwa matumizi ya vifaa hivi vya kidijitali kielimu, kikazi, kimawasiliano, kiutafiti na kadhalika. Watoto hawatapata faida hizo wakizuiwa kabisa.

Kwa upande mwingine, hata ukimzuia mtoto nyumbani, atakutana na vifaa hivi kwa jirani, marafiki, na mtaani. Lipi bora, atumie chini ya maelekezo na usimamizi wako au akajifunze mtaani?

Kutambua uwepo wa dunia ya kidijitali

Ni dhahiri kwamba watoto wa leo wanaishi katika dunia iliyounganishwa. Vifaa kama simu, kompyuta kibao na kompyuta vinakuwa sehemu ya mchakato wao wa kujifunza na kuwasiliana. Hivyo basi, wazazi na walimu hawapaswi kuona vifaa hivi kama adui, bali kama zana ambayo, ikiwa itatumika vyema, inaweza kuwasaidia watoto kukuza ujuzi wa maisha, maarifa na ubunifu.

Kwa nini si busara kuzuia kabisa?

Kuizuia teknolojia kabisa kwa watoto si suluhisho dhabiti kwa sababu aghlabu huleta migogoro kati ya wazazi na watoto, hasa kwa vijana wanaoelekea utu uzimani ambao hujisikia wamenyimwa uhuru.

Kwa upande mwingine, kwa kiasi kikubwa, mafanikio ya kimaisha ya watoto wetu katika dunia kimasomo, kikazi, na hata katika nyanja nyingine, inategemea umahiri wa kutumia nyenzo hizi. Kumzuia mwanao ni kumkandamiza kifursa.

Kwa hiyo, badala ya kuzuia kabisa watoto, ni muhimu kuelekeza matumizi kwa namna inayowafaidisha.

Jukumu la shule na familia

Shule zina jukumu la kujumuisha ujuzi wa kidijitali katika mitaala, kufundisha wanafunzi utambuzi wa habari, maadili mtandaoni, na uwezo wa kutambua habari potofu. Kwa kufanya hivyo, shule zinawapa watoto zana za kuchambua, kutathmini chanzo cha taarifa na kutengeneza maamuzi sahihi kuhusu kile wanachokiona mtandaoni.

Familia nazo zitoe msingi wa maadili na ushauri kwa watoto. Badala ya kuhukumu kila matumizi ya kidijitali, wazazi wazungumze kwa uwazi na watoto kuhusu uzoefu wao mtandaoni. Kufanya hivyo kunajenga uaminifu na kuwafanya watoto nao kufunguka.

Mazingira salama ya kidijitali

Moja ya njia bora za kuelekeza matumizi ni kutengeneza mazingira salama ya kidijitali nyumbani na shuleni. Hii inajumuisha kuweka mipaka ya muda, kuchagua maudhui yanayofaa kwa umri wa mtoto, na kufundisha jinsi ya kutumia huduma za ulinzi. Kwa kufanya hivyo, teknolojia inakuwa chombo cha kujifunza badala ya kuwa chanzo cha hatari.

Wazazi pia wanaweza kutumika kama mfano bora kwa watoto wao kwa kuonyesha jinsi ya kutumia teknolojia kwa njia yenye tija — kwa mfano, wazazi watumie programu za kielimu na kuzitumia kujifunza pamoja na watoto jambo lolote jipya. Hii inawajenga watoto uwezo wa kujisimamia vizuri mitandaoni.



Faida za matumizi mazuri kwa watoto

Kwa kutumia vifaa vya kidijitali vya mawasiliano, watoto chini ya maelekezo ya wazazi watakua kiujuzi na kifikra. Watatumia mitandao kutafuta habari zenye zenye na kujenga uwezo wa kuchambua na kufikiri kwa kina.

Pili, kutumia vifaa vya kidijitali kunakuza upendo, ukaribu na maongezi. Hii hutokea pale wazazi na shule wakiamua kutumia mitandao kuanzisha mijadala kuhusu masuala ya kijamii, taaluma na maadili.

Mapitio ya kitabu: Sanaa ya Kujitenga (The Art of Detachment)

The Art of Detachment ni kitabu cha maendeleo binafsi kilichoandikwa na Shubham Kumar Singh na kuchapishwa tarehe 30 Aprili 2025. Kitabu hiki kinachunguza kwa kina dhana ya "detachment" au kujitenga kihisia kwa njia chanya.

Mwandishi anafafanua kuwa kujitenga kihisia si kukimbia maisha wala kuwa mtu baridi, bali ni uwezo wa kuishi kwa utulivu bila kutegemea matokeo, watu au hali fulani ili uwe na amani.

Hoja kuu ya kitabu ni kwamba mateso mengi ya binadamu hayatokani na hisia zenyewe, bali yanatokana na kung'ang'ania. Watu hushikilia mahusiano, matarajio na taswira zao binafsi kana kwamba kupoteza ni janga lisilovumilika.

Mwandishi anaonyesha kuwa uhuru wa kweli huanza pale mtu anapoacha kuunganisha amani yake na matokeo ya nje. Hapo ndipo mtu anaweza kupenda, kujali na kujitahidi bila kuogopa kupoteza.

Katika sura ya kwanza, "Freedom Begins Within", mwandishi anaweka msingi kwamba kujitioa kihisia si kuacha maisha au kuwa baridi. Ni kusimama imara ndani ya maisha bila kutikisika na kila kinachobadilika.

Anasema kitu kilicho "chako kweli" hakihitaji nguvu, kulazimisha, au kubembeleza. Hapa msomaji anakumbushwa kwamba bado unaweza kupenda, kujali na kujitahidi, lakini usiunganishe amani yako na matokeo. Huu ni ujumbe unaoleta nguvu ya ndani, hasa kwa mtu ambaye huzidiwa na hofu ya kupoteza.

Sura ya pili, "Letting Go Is Not Losing", inavunja imani kwamba kumiliki ndiko usalama. Mwandishi anaonyesha kuwa maisha hayakuumbwa kumilikiwa, bali kuishiwa. Tunachoka tunapojaribu kuyafungia muda, kuwalinda watu wabaki kama walivyokuwa, au kujaribu kurudisha hali iliyopita.

Kujitenga kihisia hapa inaelezwa kama kukomaa kihisia: kuachilia hakufuti upendo, bali kunauweka safi. Kunatoa hofu, matarajio na udhibiti, na kuacha heshima, shukrani na amani. Hivyo, kitabu kinawafariji wanaopitia maumivu ya kuachwa au mabadiliko yasiyotabirika.

Sura ya tatu, "Observe, Don't Absorb", ni sehemu yenye mafunzo ya moja kwa moja ya kisaikolojia. Inatofautisha kati ya kuwa na ufahamu wa hisia na kuwa mateka wa hisia. Mwandishi anashauri: tazama mawazo na mihemko bila kuimeza.

Wazo ni kwamba hisia zinaweza kupita kama wingu, na mawazo yanaweza kuja na kuondoka bila kuwa utambulisho wako.

Kwa hiyo, unaweza kuhisi hasira bila kuwa "hasira," na unaweza kuhisi hofu bila kuwa "mwenye hofu." Ukipunguza mwitikio wa haraka, unaanza kuchagua kwa busara. Hapa kitabu kinaongea sana na vijana na watu wanaopambana na msongo wa mawazo au kujilaumu.

Sura ya nne, "Release Expectations," inaonyesha namna matarajio yanavyozalisha mateso kimya kimya. Matarajio hugeuza tumaini kuwa presha, na uwezekano kuwa kuvunjika moyo. Tunajifunga si kwa uhalisia, bali kwa picha ya jinsi tunavyodhani mambo "yanatakiwa" kwenda.

Kujitoa kihisia kunapoingia, unalegeza mkono. Unaruhusu maisha yashangaze, huku ukibaki thabiti ndani. Hii haimaanishi kushusha viwango; ina maana ya kuinua ufahamu na kukutana na uhalisia kama ulivyo.

Sura ya tano, "Choose Inner Freedom", inafunga kwa wito wa kujiongoza. Mwandishi anasema mradi furaha inategemea watu, matokeo au uthibitisho wa wengine, basi uhuru wako huwa wa masharti. Detachment huondoa masharti hayo. Unajifunza kujibu badala ya kuitika kwa pupa, kuchagua utulivu badala ya msukumo, na kuweka uongozi wa nafsi mbele.

Nguvu ya kitabu hiki ipo kwenye lugha yake nyepesi, ujumbe wake unaotuliza, na msisitizo kwamba detachment si kutopenda, bali ni kupenda bila hofu na bila minyororo. Mapungufu yake madogo ni kwamba kinatoa falsafa na tafakari zaidi kuliko mifano mingi ya maisha halisi au mazoezi ya hatua kwa hatua.

Hata hivyo, kwa mtu anayehitaji mtazamo mpya wa kuishi kwa amani katika dunia yenye mabadiliko, The Art of Detachment ni kitabu cha kusoma polepole na kutafakari kila sura.

Mitego saba ya viongozi wapya katika siku 90 za mwanzo

Siku 90 za mwanzo katika nafasi mpya ya uongozi ni kipindi nyeti sana. Ndicho kipindi ambacho taswira ya kiongozi huanza kujengwa, imani ya timu huanza kupimwa, na mwelekeo wa uongozi huanza kuonekana. Utafiti wa Profesa Michael D. Watkins, mtaalamu wa uongozi na mabadiliko ya mashirika, unaonyesha kuwa viongozi wengi hushindwa au hupoteza mwelekeo mapema si kwa kukosa uwezo, bali kwa kuangukia mitego ya kawaida katika miezi yao mitatu ya mwanzo. Ifuatayo ni mitego mikubwa saba ya uongozi katika siku 90 za kwanza, pamoja na namna ya kuiepuka.

Uchumi wa nchi unapimwaje?

UKHTI FATIMA SS

Je, umewahi kusikia habari zikisema "uchumi umekua kwa asilimia fulani" au "mfumuko wa bei umeongezeka"? Kauli kama hizi hutokana na viashiria vya uchumi. Lakini kwa mtu wa kawaida, uchumi wa nchi unawezaje kupimwa? Makala hii inakueleza kwa lugha rahisi namna ya kutathmini afya ya uchumi wa taifa lolote.

Viashiria vya uchumi ni nini?

Viashiria vya uchumi ni takwimu zinazotolewa na serikali au taasisi za kimataifa kama Benki tya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF). Takwimu hizi huonesha hali ya ukuaji, ajira, bei za bidhaa, biashara ya kimataifa na mambo mengine muhimu yanayoathiri maisha ya wananchi.

Kwa kifupi, viashiria hivi ni kama vipimo vya afya ya uchumi – sawa na jinsi daktari anavyopima shinikizo la damu au joto la mwili.

Mosi, angalia ukuaji wa uchumi (GDP)

Kipimo kikubwa cha uchumi huitwa Pato la Taifa (GDP). Hii ni jumla ya thamani ya bidhaa na huduma zote zinazozalishwa nchini kwa mwaka. Uchumi wa Tanzania unapokua, maana yake uzalishaji unaongezeka – iwe ni kwenye kilimo, viwanda, madini, utalii au huduma.

Kwa mfano, kama sekta ya utalii inapata wageni wengi zaidi au migodi inazalisha madini mengi, GDP huongezeka. Ukuaji wa wastani wa asilimia 4 hadi 6 kwa mwaka mara nyingi huonekana kuwa mzuri kwa nchi kama Tanzania. Lakini ni muhimu kujiuliza: je, ukuaji huo unawanufaisha wananchi wengi au ni sekta chache tu?

Pili, tazama mfumuko wa bei

Mfumuko wa bei ni kupanda kwa bei za bidhaa na huduma. Ukienda sokoni na kugundua bei ya sukari, mchele au mafuta ya kupikia imepanda sana, hiyo ni dalili ya mfumuko wa bei.

Kwa Tanzania, kiwango cha mfumuko wa bei kinapokuwa chini ya asilimia 5, mara nyingi huchukuliwa kuwa kinadhibitika. Bei zikipanda sana, maisha huwa magumu kwa wananchi kwa sababu mshahara hauongezeki kwa kasi sawa na bei. Hivyo, mfumuko wa bei mdogo na wa wastani ni ishara ya uchumi wenye afya.

Tatu, angalia ajira na biashara ndogo ndogo

Afya ya uchumi pia huonekana kupitia ajira. Je, vijana wanapata kazi? Je, biashara ndogo ndogo zinafunguliwa au zinafungwa?

Tanzania ina idadi kubwa ya vijana. Ikiwa wahitimu wa vyuo wanapata ajira au wanajiajiri kupitia kilimo, bodaboda, biashara au viwanda vidogo, hiyo ni dalili nzuri. Lakini kama wengi wanamaliza shule bila kazi, inaonyesha uchumi hauzalishi fursa za kutosha.

Nne, chunguza thamani ya shilingi

Thamani ya shilingi ya Tanzania ikilinganishwa na dola ya Marekani ni kiashiria kingine. Ikiwa shilingi inashuka sana, bidhaa zinazoagizwa kutoka nje kama mafuta, magari au vifaa vya hospitali hupanda bei.

Shilingi ikiwa imara kwa muda mrefu huonesha kuwa uchumi uko kwenye usawa mzuri wa biashara na fedha za kigeni. Lakini kushuka kwa thamani kunaweza kuathiri gharama za maisha.

Tano, angalia biashara ya nje

Tanzania huuza nje bidhaa kama dhahabu, korosho, kahawa, tumbaku na mazao mengine. Pia huuza gesi na hupokea watalii. Ikiwa mauzo ya nje yanaongezeka, nchi hupata fedha nyingi za kigeni. Je, nchi inauza zaidi nje kuliko inavyoagiza? Je, wawekezaji wa kigeni wanawekeza nchini? Uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje (FDI) huonesha imani ya kimataifa katika uchumi wa nchi.

Sita, tathmini miradi ya maendeleo

Miradi mikubwa kama reli ya kisasa (SGR), bwawa la umeme la Julius Nyerere, barabara na bandari huonesha jitihada za kukuza uchumi. Miradi hii huongeza ajira na kuboresha miundombinu.

Hata hivyo, ni muhimu kuangalia kama miradi hiyo inaleta faida kwa wananchi na kama deni la taifa linaongezeka kupita kiasi. Deni likiwa kubwa sana, linaweza kuwa mzigo kwa vizazi vijavyo.

Saba, chunguza deni la taifa na matumizi ya serikali